# MABADILIKO YA NAFASI NA MTAZAMO WA WAHUSIKA WANAUME KATIKA RIWAYA ZA SAID A. MOHAMED: *UTENGANO* (1980) NA *DUNIA YAO* (2006)

**NA**

**MWANGI TERESIA WANJIKU**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI, KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**2018**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

______________________ __________________________

MWANGI TERESIA WANJIKU TAREHE
C50/CE/22325/2010

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi

PROF. CATHERINE NDUNGO TAREHE

DKT. PAMELA M.Y. NGUGI TAREHE

## SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema ya kukamilisha kazi hii.

Nawashukuru pia wasimamizi wangu Profesa Catherine Ndungo na Dkt. Pamela Ngugi kwa kutenga muda wao ili wanielekeze katika kila hatua na hivyo nikaimaliza kazi hii. Mola awabariki sana.

Aidha, shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika, hasa wale waliongoza masomo yangu ya shahada ya uzamili hadi nikafanikiwa. Hakika, mchango walioutoa Profesa King'ei, Dkt. Wafula na Dkt. Chacha ulinisaidia mno. Mungu awazidishie upendo huo.

Nashukuru Chuo cha Kenyatta kwa kunipa fursa ya kuendeleza masomo yangu ya shahada ya uzamili.

Vile vile nawashukuru wanafunzi wenzangu hasa Sista Celestine Katuka, Benson Ngige, Philomena na Mercy Kamachu kwa kunishauri, kunitia moyo na kunihimiza niikamilishe kazi hii.

Nawashukuru pia wazazi wangu wapendwa kwa kunitia moyo kila mara na kuniombea nikamilishe kazi hii.

Aidha,namshukuru kwa dhati mume wangu Wilson Ngugi kwa kunitia moyo na kunitimizia mahitaji ya kifedha wakati wa kufanya kazi hii. Mwisho namshukuru mwanangu John Ngugi kwa uvumilivu mwingi wakati wa masomo yangu.

# TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu mpendwa Wilson Mwangi na mwanangu John Ngugi.

## YALIYOMO

**MADA** **UKURASA**

UNGAMO……………………………………………………………..............i

SHUKRANI ………………………………………………………………ii

TABARUKU ………………………………………………………..…. iii

YALIYOMO…………………………………………………….............iv

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU...……………………….............viii

VIFUPISHO ………………………………………………………………ix

IKISIRI……………………………………………………………………x

ABSTRACT………………………………………………………..…xi

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi…………………………………………………………….1

1.1 Usuli…………………………………………………………………….1

1.2 Suala la utafiti ……………………………………………………..3

1.3 Maswali ya utafiti ………………………………………………...4

1.4 Malengo ya utafiti….………………………………………………4

1.5 Sababu za kuchagua mada………………………………………………5

1.6 Upeo na mipaka ……………………………………………………...6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ………………………………………...7

1.7.1 Hitimisho…………………………………………………………..13

1.8 Misingi ya nadharia …………………………………………………14

1.8.0 Historia fupi ya nadharia ya uhalisia…………………………………14

1.8.1. Nadharia ya uhalisia katika mawanda ya fasihi……………………...14

1.9 Mbinu za utafiti ……………………………………………………...19

1.9.1 Muundo wa utafiti …………………………………………………20

1.9.2 Mahali pa utafiti …………………………………………………...20

1.9.3 Uteuzi wa sampuli………………………………………………….20

1.9.4 Ukusanyaji wa data………………………………………………...20

1.9.5 Uchanganuzi wa data...……………………………………………..21

1.9.6 Uwasilishaji wa data...……………………………………………….21

**SURA YA PILI: Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume**

2.0 Utangulizi……………………………………………………………22

2.1Mabadiliko ya nafasi…………………………………………………22

2.1.1 Mtafuta riziki………………………..……………………………..22

2.1.2 Mtunga sheria na mdhibiti familia ………………………………...24

2.1.3 Mtafuta suluhisho la matatizo na asiyekata tamaa……………………29

2.1.4 Mfanya kazi za nje bali si ndani ya nyumba………………………….32

2.2 Mabadiliko ya mtazamo……………………………………………...34

2.2.1 Mtazamo kuhusu uhuru wa mwanamke………………………………34

2.2.2 Mtazamo kuhusu ukwasi na madaraka………………………………..36

2.2.3 Mtazamo kuhusu kazi na malipo halali……………………………….38

2.3  Hitimisho…………………………………………………………….40

**SURA YA TATU: Sababu za mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume**

3.0 Utangulizi…………………………………………………………………...41

3.1 Historia fupi ya Mwandishi Said A. Mohamed………………………….41

3.2 Sababu za mabadiliko ya nafasi na mtazamo……………………………42

3.2.1 Mabadiliko ya kimazingira…………………………………………….42

3.2.2 Mabadiliko ya kijamii………………………………………………….44

3.2.3 Mabadiliko ya kiuchumi……………………………………………….48

3.2.4 Mabadiliko ya kisiasa………………………………………………….50

3.3 Hitimisho……………………………………………………………...51

**SURA YA NNE: Athari za mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui**

4.0 Utangulizi ………………………………………………………………..53

4.1 Mmomonyoko wa maadili……………………………………………….53

4.1.1 Watoto kuwakosea wazazi heshima……………………………………54

4.1.2 Uasherati………………………………………………………………..55

4.1.3 Matumizi ya dawa za kulevya…………………………………………57

4.2 Ukosefu wa kazi na athari zake………………………………………….58

4.3 Kukata tamaa maishani…………………………………………………..61

4.4 Kukita mizizi kwa ukoloni mamboleo…………………………………...62

4.5 Malezi…………………………………………………………………….65

4.6 Mapenzi……………………………………………………………….66

4.7 Nafasi mpya ya mwanamke……………………………………………...68

4.8 Kutengana na kusambaratika kwa familia……………………………….71

4.9 Utandawazi na athari zake……………………………………………….73

4.10 Hitimisho……………………………………………………………….75

**SURA YA TANO: Muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti**

5.0 Utangulizi……………………………………………………………..76

5.1 Muhtasari……………………………………………………………...76

5.2 Matokeo……………………………………………………………….77

5.3 Mchango wa utafiti……………………………………………………84

5.4 Changamoto…………………………………………………………...84

5.5 Mapendekezo……………………………..…………………………...84

# UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Mfumo wa kuumeni-** Utaratibu wa kijamii, kisiasa na kiuchumi unaohakikisha, kuhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanamume katika nyanja zote za maisha. Hujitokeza bayana katika familia za kuumeni ambapo mwanamume ndiye kiongozi wa familia.

**Jinsia-** Hali ya kimaumbile ya mtu kuwa kike au kiume.

**Uana-** Utaratibu wa kijamii unaoimarisha tofauti za matarajio na majukumu kati ya wake na waume katika jamii.

**Utandawazi** - Upanuzi wa mahusiano na maingiliano ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kitamaduni baina ya mataifa hivi kwamba ulimwengu huwa kama kijiji kidogo. Upanuzi huu huwezeshwa na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanayofanya mataifa ya jamii kuwasiliana kwa urahisi.

**Ulimbwende** – Mwelekeo wa kusimulia ambapo wahusika huwa mashujaa na wenye nguvu za ajabu.

## VIFUPISHO

Uk. - Ukurasa

I.L.O.- International Labour Office

W.E.F. – World Economic Forum

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya mbili teule za Said A. Mohamed:*Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006). Utafiti umebanisha kwamba kuna mabadiliko katika nafasi zao kwenye jamii hasa katika familia. Pia, mtazamo wao kuhusu wanawake na masuala mbalimbali katika maisha umebadilika. Aidha utafiti ulionyesha sababu zilizochochea kuzuka kwa mabadiliko hayo katika kusawiri wahusika wanaume. Ni wazi kuwa fasihi huchota mali ghafi yake kutoka kwa jamii na hivyo hali za kiuchumi, kisiasa, kijamii na vile vile tajriba yake mwandishi kwenye mazingira anamoishi, huathiri uandishi wake. Pia, utafiti ulijaribu kuonyesha athari za mabadiliko hayo katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui. Ili kutekeleza hayo, tuliongozwa na nadharia ya uhalisia iliyoasisiwa na Gustave Flaubert na wengineo. Nadharia hii inajikita kwenye vitu thabiti vinavyohisika na mishipa ya fahamu ya mwanadamu na pia ukweli unaodhihirika katika kazi ya fasihi. Uhalisia wa kifasihi huonyesha uwezo wa kazi ya fasihi kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Kupitia kwa nadharia hii, ni wazi kuwa uhalisia wa mazingira anamoishi mwandishi na hata tajriba yake kwenye mazingira hayo, humwathiri pakubwa kwenye uandishi wake kama vile jinsi anavyowachora wahusika wake. Utafiti huu ni wa kimaelezo na ulifanyiwa maktabani. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia mbinu kusudio kwani ililenga vitabu mahsusi vya riwaya vinavyoonyesha mabadiliko hayo. Mtafiti alisoma kwa kina riwaya teule, vitabu, makala, majarida, tasnifu na hata tafiti na makala mtandaoni yenye ukuruba na mada ya utafiti huu. Aidha, vitabu na tafiti zilizofanywa kuhusiana na nadharia ya uhalisia zilisomwa. Baada ya kukusanya data na kuichanganua kutegemea malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia, mtafiti aliwasilisha matokeo kwa njia ya maelezo kwenye sura mbalimbali. Mtafiti anakisia kuwa matokeo ya utafiti huu yatadhihirisha kuwa mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume yalisababishwa na mabadiliko ya mazingira alimokulia na alimoishi mwandishi, mabadiliko ya kijamii, kisiasa na hata tajriba na ukuaji wake kama mwandishi. Inatarajiwa kuwa wasomi, waandishi wa fasihi na hata watafiti wa kifasihi watanufaika kutokana na kazi hii.

## ABSTRACT

This research focused on the change of male characters' role and their view as seen in two selected novels, *Utengano* (1980) and *Dunia Yao* (2006) by Said A. Mohamed. It clearly shows that men's role has changed in the society and especially in families. Furthermore, their view of women and other life issues has greatly changed. The research also explains the reasons that triggered those changes. It's evident that the things talked about in literature are gotten from the society hence economic, political and social situations and also the author's gained experience affect his work. The effects of these changes on the theme development of the novel are also explained. The research was guided by the realism theory that was pioneered by Gustave Flaubert and others. This theory puts across facts, real life issues and things perceived by human senses. Reality in literature is the ability to interpret and describe various happenings that occur in real life. Through this theory, it's evident that reality of the place where the author lives and his experience affects his work of writing through the ways he or she portrays his or her characters. This is a descriptive research and it was carried out in the library. Data for this research was mainly obtained by reading the selected texts, other books, journals, thesis and internet research relevant to this study. Books and research done on realism theory were also read. After collecting data and analyzing it being guided by the aims of the research and tenets of realism theory, findings were presented by descriptive method in various chapters. The researcher estimates that the findings of this research will reveal that change of male characters' role and their view was caused by changes in the environment in which the author grew and lived, social and political changes and even the authors experience and development as an author. It is expected that this study will be useful to scholars, authors and also researchers in literature.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia vipengele vya kimsingi vya utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni kama vile usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada miongoni mwa vipengele vingine muhimu.

## 1.1 USULI

Bakhtin (1986) na King'ei (2000: xv) wanakubaliana kuwa fasihi hukua, hubadilika na kuathirika kutokana na hali mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hivyo, kazi yoyote ya fasihi inatazamiwa kubadilika wakati wowote na haiwezi kuwekewa sheria. Aidha, fasihi ni kioo cha jamii na hivyo malighafi ya fasihi hutolewa kwenye mazingira halisi na hali halisi za kiuchumi, kisiasa, kisaikolojia, kijamii na hata tajriba aliyopata mwandishi kwenye mazingira yake. Zaidi ya hayo, kuwepo na kudumu kwa kazi ya kisanaa hutegemea ubunifu na upya wa aina fulani (Mohamed, 2008).

Harrow (1994) anasema kuwa fasihi ya Kiafrika katika karne ya ishirini imekua na kutoka katika ushairi wa asili wa hapo awali wa kinegritudi (ujitambuzi wa Mwafrika) hadi kufikia riwaya za sasa za hivi majuzi za uhalisiaajabu. Waandishi wa riwaya na mashairi walipoendelea kushuhudia mambo ya kipekee katika maisha yao na jamii zao, mikakati mipya ya uandishi ilianza kujitokeza. Swala hili la mabadiliko lilijitokeza katika kazi za waandishi waliokabiliwa na migogoro ya jamii zao na kukusudia kuanzisha utaratibu mpya wa kijamii na kitamaduni. Maelezo haya yote yanadhihirisha wazi kuwa mambo yanayomzingira mwandishi yeyote yule katika mazingira tofauti humwathiri sana katika uandishi wake.

Utafiti huu ulichunguza sababu zilizoathiri mwandishi Mohamed kuzua mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya zake teule. Nia ya utafiti huu ilikuwa ni kuonyesha mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika fasihi ya Kiswahili. Riwaya zilizoshughulikiwa ni *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006) za Said A. Mohamed. Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume yanajitokeza wazi kwa kulinganisha riwaya moja ya miaka ya themanini na nyingine ya miaka ya sasa ya elfu mbili na kuendelea. Nia ya utafiti huu ilikuwa ni kuweka wazi mabadiliko haya, kujaribu kuelezea sababu za mabadiliko hayo na pia athari za mabadiliko hayo katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui.

Izingatiwe kuwa Mohamed, ambaye ni mzaliwa wa Unguja (Zanzibar), aliwahi kusomea, kufanya kazi na kuishi katika sehemu mbalimbali za ulimwengu huu zenye matukio na tamaduni tofauti kukiwemo Dar es Salaam, vyuo vikuu vya Moi (Eldoret), Nairobi, Leipzig (Ujerumani), Osaka (Ujapani) na Bayreuth (Ujerumani).

Irele (2009) anaangazia riwaya ya Kiafrika na kuandika kuwa ingawa Afrika imekuwa na historia ndefu ya ushairi na mchezo wa kuigiza, leo hii riwaya ndio utanzu unaotawala takriban kila mahali ulimwenguni. Ujuzi wa kusoma na kuandika ulileltwa kwa mara ya kwanza Afrika na Waarabu. Hii ilikuwa kabla ya kuja kwa Wazungu. Uwepo wa Waarabu Afrika Kaskazini ulisababisha kusambaa kwa dini ya Uislamu katika mataifa mengine ya Afrika. Hivyo, Koran takatifu ilikuwa inarejelewa sana katika taratibu za uandishi wa fasihi.

Ayang (1970) anatafiti kuhusu historia ya Zanzibar na kusema kuwa, ukoloni katika nchi hiyo ulikuwa wa mara mbili yaani wa Waarabu na kisha wa Waingereza. Tawala hizi ziliathiri jamii ya visiwani kwa namna tofauti. Kwa mfano, Waarabu walileta hati ya Kiarabu. Nao utawala wa kibepari ulioletwa na Wazungu ulivunja muundo wa kijamii visiwani na kuimarisha muundo wa

kitabaka. Kulingana na Mrina na Mattoke (1980), Waafrika waliachwa katika hali ya umaskini na dhiki. Walikuwa watumwa, wakwezi, wakulima wadogo na watumishi katika majumba ya wakoloni. Wakati huo juhudi za watunzi zilionekana walipotunga riwaya na mashairi ya kimapambano ili kutia shime raia dhidi ya unyanyasaji kama huo. Baada ya Afrika Mashariki kupata uhuru, raia waligundua kuwa uhuru waliopata ulikuwa wa bendera tu. Viongozi wapya Waafrika walijaa ulafi na ubinafsi. Basi waandishi kama Said A. Mohamed wakaandika riwaya na mashairi kuwasuta viongozi hao. Aidha mwandishi huyu amefanya kazi kwa muda mrefu katika nchi za nje zilizoendelea sana. Huenda ikawa aliathirika kiutunzi kutokana na mazingira hayo na hili lilikuwa ni jukumu la utafiti huu kuchunguza hayo. Shaka (2013) katika athari za utandawazi barani Afrika anasema kuwa, utandawazi umeleta mabadiliko mengi kwa mfano mawasiliano kurahisishwa na kuharakishwa, kupotea kwa tamaduni za kale na kuja kwa tamaduni za kigeni hasa mijini.

Riwaya zilizoteuliwa kutumika katika utafiti huu ni za nyakati mbili tofauti ambapo *Utengano* ni ya miaka ya themanini baada ya ukoloni na *Dunia Yao* ni ya miaka ya sasa ya elfu mbili kuendelea. Hivyo mkabala huu ulikuwa mwafaka katika kuonyesha mabadiliko ya nafasi na mitazamo ya wahusika wanaume. Utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia ambayo huzingatia namna ukweli ulivyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Kila kizazi huwa na ukweli au uhalisia wake unaodhihirika katika fasihi.

## 1.2 SUALA LA UTAFITI

Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Kila jamii huwa na wanawake na wanaume na fasihi ni kioo cha jamii kwa hivyo huchota malighafi yake kwenye mazingira halisi. Katika maisha, wanaume wana nafasi muhimu katika jamii za Kiafrika kwenye sekta ya uchumi, siasa na hata jamii. Tafiti

kadha za riwaya ya Kiswahili zimefanywa kuchunguza usawiri wa wahusika kwa mfano Muindi (1990), Sirucha (1986), Ndungo (1985), Gitau (2005) na Mavisi (2007). Hata hivyo, nyingi ya tafiti hizi zimelenga usawiri wa wahusika wanawake. Kadri mtafiti ajuavyo, mabadiliko yanayobainishwa na riwaya ya Kiswahili katika usawiri wa wanaume hususan nafasi na mtazamo wao hayajachunguzwa. Kazi yoyote ya fasihi inatazamiwa kubadilika wakati wowote na haiwezi kuwekewa sheria. Mabadiliko huwa ni katika uteuzi wa mada, usawiri wa wahusika na hata mbinu za kimtindo.

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

a) Ni mabadiliko yepi ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume yamedhihirika katika riwaya teule za Mohamed Said?

b) Mabadiliko hayo yamesababishwa na nini?

c) Mabadiliko hayo yana athari gani katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui?

## 1.4 MALENGO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo yafuatayo:

a) Kuonyesha mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume kama yalivyodhihirika katika riwaya teule.

b) Kuonyesha sababu za mabadiliko hayo.

c) Kubainisha athari za mabadiliko hayo katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Wahusika ni nguzo muhimu katika kazi yoyote ile, iwe ni fasihi au matini zilizopata kuandikwa na wasanii. Ijapokuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu usawiri wa wahusika katika fasihi ya Kiswahili, watafiti wengi wamejikita sana kwenye wahusika wanawake. Mshawasha wa kuchagua mada hii ulitokana na sababu kuwa tafiti zilizofanywa kumhusu mwanamke, zimemchora mwanamme kama mwenye kudharau, kunyanyasa, kupuuza na kudunisha mwanamke. Utafiti huu ulinuia kuchunguza ikiwa bado mwanamume yuko hivyo au nafasi na mtazamo wake umebadilika na sababu za mabadiliko hayo.

Aidha, baadhi ya watafiti kama vile Wandera (2002), Kimani (2003) na King'ei (2002) wanapendekeza kuwa utafiti ufanywe kwa kuangalia wanaume kwani mengi tayari yametafitiwa kuhusu wanawake. Zaidi ya hayo, Wandera (2002) anasema kuwa tafiti za kijinsia katika fasihi ya Kiswahili zitadumu kadri mwanadamu anavyozidi kuwepo. Tafiti hizi zitakua na kubadilika kulingana na mahitaji ya kijinsia ya jamii husika, muktadha na kipindi husika cha kihistoria na hivyo tafiti hizi ni muhimu.

Utafiti huu ulijikita kwenye riwaya za Mohamed kwa sababu zimechambua kwa undani jamii na kukadiria jinsi maisha ya jamii nyingi za ulimwengu wa tatu yalivyo. Mwandishi huyu ana uwezo wa kuibua hali halisi na pia kazi zake hazijajikita kwenye jamii finyu ila zinahusu jamii pana. Riwaya zilizochaguliwa zina uwezo wa kudhihirisha kwa utoshelevu mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume kwa kuangalia moja ya miaka ya themanini na moja ya karne ya ishirini na moja. Hizi ni nyakati mbili tofauti zenye matukio tofauti ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa.

Riwaya ya *Utengano* iliandikwa baada ya Unguja kujinyakulia uhuru na ukoloni mambo leo kuanza kuendelezwa na viongozi Waafrika. *Dunia Yao* iliandikwa katika kipindi ambapo nchi za Afrika zilikuwa zinapitia athari nyingi za kigeni mfano utandawazi. Kutokana na utafiti huu, wasomi wa fasihi andishi watapata tajriba mpya kuhusiana na masuala ya uana. Pia matokeo ya utafiti huu yatawafanya wapenzi wa fasihi kutosoma juu juu kuhusu wahusika bali kujaribu kutafuta kiini cha wahusika hao kusawiriwa hivyo kutegemea waandishi husika na mabadiliko katika maisha halisi.

**1.6 UPEO NA MIPAKA**

Utafiti huu ulijikita kwenye riwaya mbili yaani *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006) za Said A. Mohamed. Huyu ni mwandishi aliyeandika riwaya nyingi, ushairi, tamthilia, hadithi fupi na hata mikusanyiko ya fasihi simulizi. Riwaya hizo ziliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha wakati wa kuchapishwa kwazo. Kigezo hicho ni muhimu katika kubainisha mabadiliko na sababu za mabadiliko hayo katika nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume kupitia vipindi tofauti vya kihistoria yaani miaka ya themanini na karne ya ishirini na moja. Mabadiliko ya nafasi yaliyolengwa ni kuhusu majukumu ya mwanaume katika familia na pia hulka yake. Nayo mabadiliko ya mtazamo yaliangazia uhuru wa mwanamke wa kutoka nje, mtazamo kuhusu ukwasi na madaraka na pia kazi na malipo halali.

Hill (1977) anatoa maoni kuwa usawiri bora wa wahusika huhitaji hali ya juu ya ubunifu ili kuwafanya wahusika hao wadhihirishe hali halisi zinazopatikana katika mazingira ya kawaida. Riwaya mbili ziliteuliwa kwani zina mawanda mapana ya kuweza kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Ijapokuwa wahusika katika riwaya mbili teule ni wengi, kwa jumla wahusika kumi na wawili waliangaziwa. Hawa waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha jinsia na pia mchango wao mkubwa katika kutosheleza madhumuni ya utafiti huu ya kubainisha mabadiliko ya nafasi na

mtazamo wa wahusika wanaume. Hii ni kwa sababu, matukio yaliyowazunguka yalihusiana kwa karibu na mada ya utafiti huu hivyo kuwa muhimu katika kutupa data. Kati ya hao kumi na wawili, wawili ni wahusika wakuu. Wanahusishwa na takriban visa vyote katika riwaya kutoka mwanzo hadi mwisho. Wahusika wengine saba ni wasaidizi waliotumika kuwajenga wahusika wakuu. Aidha, wao ni aila za wahusika wakuu. Hao wengine watatu ni wahusika wadogo kwani wameendeleza suala lengwa kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na wahusika wakuu. Aidha wahusika hawa wote waliteuliwa kutokana na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Wa Thiong'o (1972), Senkoro (1988) na Njogu na Chimerah (1999) wanaafikiana kuwa kazi yoyote ya fasihi haizuki kwenye ombwe tupu bali huwa ni mkururo wa tajriba za mwandishi pamoja na kadhia zilizomsibu mfano ukoo na aila yake, malezi, elimu, mazingira alimokulia, ndoa zake, matukio ya kijamii na historia, mikondo ya siasa na utawala, itikadi zake na fauka ya yote, matamanio, falsafa na ndoto zake katika maisha. Hivyo, fasihi hupewa mwelekeo, umbo na umuhimu wake na masuala ibuka katika jamii mahususi. Mabadiliko yatokeayo katika nyanja mbalimbali zilizotajwa huathiri kazi ya fasihi kwa jumla.

Katika kipindi cha miaka michache iliyopita hasa katika ulimwengu wa ukapitalisti, baraza za wanaume, majarida na makala ya magazeti kuhusu uume yaliongezeka. Kushughulikia wanawake pekee pia kumekashifiwa na waandishi mbalimbali waliosema kuwa, kuzungumzia au kujihusisha na mambo ya kijamii kana kwamba ni suala la wanawake pekee hupotosha kwani ni suala lilo hilo ambalo ufeministi unajaribu kupigana nalo. Wandera (2002) na King'ei (2002) wanasema kuwa tafiti nyingi juu ya masuala ya uana zimemzingatia mwanamke na hivyo kuna haja ya kufanya tafiti juu ya wanaume. Katika kutafiti kuhusu wanaume, utafiti huu unalenga

kuchunguza iwapo katika riwaya ya Kiswahili, nafasi ya mwanamme na mtazamo wake kuhusu masuala tofauti ya maisha umebadilika na sababu za mabadiliko hayo.

Kwa upande mwingine, Flood (1990) anasema kuwa upinzani pia umetolewa dhidi ya kushughulikia masuala yanayohusu wanaume kwani baadhi ya watu wanaona kuwa kuyazingatia mambo hayo kutaendeleza na kudumisha dhana zilizopo za kijinsia mfano dhana kuwa wanaume wote hufaidi kutokana na maswala ya jinsia. Tunaishi katika jamii iliyojikita kwenye mfumo wa kuumeni. Inashughulikia faida au mambo yanayowapendelea wanaume. Utafiti huu unashikilia kuwa ni muhimu kuwashughulikia wanaume katika tafiti za kifasihi kwani ndiyo njia pekee ya kuwaelewa vyema na pia kuondoa dhana za uongo kuwahusu.

Morell (2005) anaeleza kwamba wafeministi wengi wanahofia kujikita kwa masuala ya wanaume kwani jambo hili linanuia kurudisha nyuma juhudi za wanawake. Wanasema kuna mabadiliko kadhaa ambayo yametokea na baadhi ya wanaume wanajizatiti kuishi kwa amani na wanawake, watoto na wao wenyewe lakini wanaume wengine wameshindwa kujitambua na kutekeleza hili. Nia ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza ukweli wa kauli hii na hasa katika jamii ya Waafrika kupitia kwa riwaya ya Kiswahili.

Katika utafiti wake, Symon (1999) anachunguza jinsi waandishi watatu wa kiume walivyowawasilisha wahusika wanaume katika riwaya zao huko Uingereza. Mahusiano kati ya wahusika hawa na wahusika wengine wanaume ambao waandishi wanaumba yaliangaziwa. Anaonyesha kuwa miaka ya 1988-1995 kazi hizi za ubunifu zilitolewa na kilikuwa kipindi ambapo tafiti kuhusu uana kurejelea wanaume zilifanywa. Aidha anaeleza kuwa ndani mwa dhana za uume huko Uropa magharibi mna kunyanyaswa kwa wanawake na kutawala kwa wanaume. Hata hivyo, wanaume hawatawali tu wanawake bali pia wanaume wengine. Kwanza,

utafiti huu ulitofautiana na wake kimazingira kwani ulilenga riwaya za Kiswahili za hapa Afrika. Aidha, utafiti wa Symon unalenga usawiri wa wahusika wanaume bila kuangazia mabadiliko kihistoria na sababu za mabadiliko hayo mfano itikadi ya mwandishi. Vile vile, utafiti huu unaangazia mwandishi mmoja na jinsi ameonyesha mabadiliko katika uwasilishaji wa wahusika kwenye riwaya zake teule.

Kama anavyosema Gagiano (2000), waandishi wengi wa riwaya aghalabu huwa ni wachanganuzi wa jamii wanazosawiri na huwa wa kimsingi katika kuwaza na kuchunguza masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa sio watu wa kurekodi tu. Utafiti wake ulitufaa katika kuchunguza sababu za mwandishi Said A. Mohamed kuzua mabadiliko katika usawiri wa nafasi na mtazamo wa wahusika wake wa kiume. Crous (2005) katika utafiti wake wa jinsi masuala ya wanaume yalivyowasilishwa katika simulizi bunifu za waandishi teule huko Afrika Kusini, baada ya kipindi cha ‘ubaguzi wa rangi’, anaonyesha jinsi wanawasilisha vipengele vya uume huko Afrika Kusini na vile wanachunguza mahusiano ya mamlaka kati ya wahusika wanaume na kike na pia maoni ya wanaume kuhusu jinsia. Mawazo haya yalitufaa katika kuchunguza iwapo wahusika wa kiume katika riwaya teule wamebadilisha mtazamo wao kuhusu wanawake na kwa njia gani.

Libby (2012) anashughulikia suala la mfumo wa kuumeni uliojikita kwenye dini ya kikristo. Mfumo huu unasisitiza utaratibu wa utawala msonge au kingazi katika familia. Ukristo unazingatia utaratibu huu kuwa umetoka au kuamuliwa na Mwenyezi Mungu. Wanawake na wanaume wana majukumu mbalimbali ya kutekeleza ambapo mume ndiye mwenye kukimu na kulinda familia naye mke ndiye wa kulea watoto na pia kushughulikia masuala ya nyumbani mfano upishi. Kulingana na mfumo huu, wanawake wanafaa kuwa chini ya utawala wa wanaume siku zote. Mabinti wanafaa kuwatii baba zao na wake wanafaa kuwatii waume wao.

Kila mmoja wao akitekeleza jukumu lake alilopewa na Mungu basi familia itastawi. Basi, mfumo wa kuumeni wa kikristo ni ile imani kuwa Mungu ameamuru na kuweka utaratibu mahususi katika familia ambao lazima ufuatwe. Mwanamume aongoze naye mke atii na kufuata. Mfumo huu una vipengele viwili muhimu. Cha kwanza ni imani katika uongozi au utawala wa kiume na kisha imani kuwa wanaume na wanawake wana majukumu tofauti kabisa ya kutekeleza. Mfumo huu unashikilia kuwa mwanamke hafai kamwe bila kuwa chini ya uongozi wa kiume. Utafiti huu unalenga kubaini iwapo utaratibu huo bado upo na iwapo umebadilika, sababu za mabadiliko hayo ni zipi.

Walby (1990) katika kuzungumzia mfumo wa kuumeni anasema kuwa ni utaratibu wa kijamii unaolenga kumtawala, kumtumia ovyo, kumnyanyasa mwanamke na kumthibiti. Viwango vya uthibiti huu hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kwa sababu ya tofauti za kitabaka, kidini, kikabila na tamaduni. Asasi ya dini ndiyo huupa nguvu mfumo wa kuumeni kwani inathamini utawala wa mwanamume zaidi katika jamii. Pia sheria kuhusu familia, talaka, ndoa na urithi zinahusishwa na mfumo wa kuumeni. Mawazo ya Libby na Walby yalitufaa kwenye utafiti huu katika kuchunguza iwapo mwandishi Mohamed ambaye ni Muislamu ameathiriwa na dini yake katika usawiri wa wahusika wake na iwapo ndiyo, sababu zilizomchochea kubadili usawiri wake wa wahusika wanaume katika *Dunia Yao* zilichunguzwa.

Katika Biblia takatifu (United Bible Societies, 1952) kwenye kitabu cha Wakorintho wa kwanza mlango wa kumi na mmoja mstari wa tatu, kichwa cha kila mwanamume ni Kristo na kichwa cha mwanamke ni mwanamume. Katika Ukristo, jinsia ya kike na kiume ni sawa lakini zina majukumu tofauti ya kutekeleza. Majukumu yote ya jinsia hizi mbili ni muhimu na hivyo basi hakuna jinsia inayoweza kutekelezea hiyo nyingine majukumu. Kulingana na mfumo huu wa

kuumeni katika Ukristo, watoto wanatarajiwa kuwatii wazazi wao kikamilifu kwa sababu kuwatii wazazi ni kumtii Mungu.

Tannen (1990) anadhihirisha kuwa mahusiano baina ya wanawake na wanaume huathiriwa na matatizo ya kisaikolojia, ukosefu wa upendo wa kweli, ubahili, athari za ukosefu wa usawa katika masuala ya kisiasa na hata kiuchumi. Wanawake huhisi kuwa ni kawaida kushauriana na waume zao kila wakati na kufanya uamuzi pamoja ilhali wanaume huhisi kuwa ni kawaida kufanya maamuzi mengi bila kushauriana na wake zao. Wanaume huhisi kuchoshwa na majadiliano marefu. Mawazo haya yalitufaa katika kuangazia mabadiliko ya nafasi ya wanaume katika riwaya teule.

Kanana (2000) alifanya utafiti kuhusu kubadili mielekeo ya wanaume wa jamii ya Ovawambo katika nchi ya Namibia kuhusu mfumo wa kuumeni na iwapo Biblia yaweza kusaidia. Katika jamii yake, uwezo na mamlaka katika familia hupokezwa mwanamume hivyo kuzua mfumo wa kuumeni. Ubaguzi wa wanawake huanza mtu akizaliwa ambapo kila mwanafamilia huhisi vibaya iwapo mtoto aliyezaliwa ni wa kike na kushangilia sana iwapo ni wa kiume. Zaidi ya hayo, mtoto wa kiume hulelewa kwa njia tofauti huku akipewa heshima sana. Hadi kufikia mwaka wa 1992, wanawake katika jamii ya Ovawambo hawakuruhusiwa kuzungumza kanisani lakini Kanana anasema kuwa hisia ya jumla imezuka siku hizi kuwa mfumo wa kuumeni ni bure. Licha ya upinzani mkubwa kutoka kwa baadhi ya watu, sheria ya nchi yake ya Namibia sasa inashikilia kuwa lazima wanawake washirikishwe vyema katika uongozi na kushika nyadhifa muhimu kuliko ilivyokuwa hapo awali. Matokeo ya utafiti wake yalifaa katika utafiti huu katika kuchunguza mabadiliko ya mtazamo wa wahusika wanaume kuhusu mtoto wa kike na wanawake kwa jumla na sababu za mabadiliko hayo.

Chaterji (2004) anachunguza mabadiliko katika mfumo wa kuumeni kama alivyofanya Kanana lakini alizingatia jamii ya Wahindi kule Uhindi. Anadhihirisha kuwa majukumu ya wanawake katika jamii hiyo yamebadilika kimfululizo katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Ingawa jambo hili halikufikirika wala kutazamika hapo awali, sasa wanachukua uongozi na mamlaka mikononi mwao. Pia anatoa mifano ya mabadiliko ya majukumu ya wanawake na wanaume. Anaeleza kisa cha wanawake watano waliodaiwa kumwua jambazi sugu. Vile vile mtu aitwae Yadau alichomwa kisu na kupigwa mawe na kundi la wanawake. Aidha, Chaterji anaonyesha athari ya mabadiliko ya kiuana hasa katika mahusiano kama ndoa yaliyosababishwa na maendeleo ya wanawake katika masuala ya kijamii, kiuchumi, kimawazo na kisiasa duniani kote. Wanaume wanaona vigumu kuishi na wanawake kama hao. Je, kupitia riwaya ya Kiswahili, mabadiliko ya nafasi ya wanaume Waafrika ni yepi na yamesababishwa na nini? Hili ni jukumu mojawapo la utafiti huu.

Amadiume (1987), mwanasosholojia kutoka Nigeria, alifanya utafiti katika kijiji chake cha Nnobi kilichoko Kusini Mashariki mwa nchi hiyo. Utafiti wake unahusu uana na jinsia katika jamii ya Kiafrika. Anatoa hoja kuwa, katika jamii ya kabla ya ukoloni jinsia na uana hazikugongana. Anachunguza miundo ambayo iliwawezesha wanawake kupata nguvu na akaonyesha kuwa majukumu hayakusemekana kuwa ya kike au kiume. Utafiti wake wa jamii ya Igbo nchini Nigeria uligawanywa katika vipindi vitatu: kipindi kabla ya ukoloni ambapo mifumo ya jadi ilitenda kazi, kipindi cha ukoloni ambapo Waingereza walitawala nchi ya Nigeria na kipindi cha baada ya ukoloni wakati nchi hiyo ilipata uhuru. Anasema kuwa wanawake wangeweza kutekeleza majukumu ambayo kwa kawaida husemekana ni ya wanaume. Hivyo basi wanawake wakaitwa ‘wanaume’. Hili liliwezeshwa na hoja kuwa wanawake hawa walijitegemea kiuchumi na pia kulikuwepo na dini iliyowaangazia wanawake. Mabadiliko ya kiuchumi wakati

wa ukoloni yalipuuza hadhi ya wanawake na kupunguza jukumu lao la utawala. Wakoloni wakaibuka na taasisi za mfumo wa kuumeni. Mawazo ya utafiti huu wa Amadiume yanafaa utafiti huu katika kuchunguza iwapo athari za nyakati mbalimbali za kihistoria mfano ukoloni, zimemwathiri mwandishi wa riwaya teule katika mabadiliko ya usawiri wa nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika kazi zake.

Gitau (2005) anachunguza suala la unyanyasaji dhidi ya wanaume katika riwaya mbili na tamthilia mbili. Aliangazia mwandishi mmoja wa kike na watatu wa kiume. Mtafiti huyo anaonyesha aina za unyanyasaji dhidi ya wanaume na misingi yake kwa mfano, kudhulumiwa kimapenzi na kupigwa. Hivyo anaangazia mambo hasi wanayotendewa wanaume. Utafiti huu ni tofauti na wake kwani kwanza, unajikita kwenye mwandishi mmoja wa kiume. Aidha unalenga kuonyesha mabadiliko katika nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume. Unajikita kwenye sehemu zote mbili yaani uhasi (mambo mabaya) na uchanya (mambo mema).

### 1.7.1 HITIMISHO

Sehemu hii imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada. Imedhihirika wazi kuwa ni vyema kufanya tafiti kuhusu wanaume kwani jamii si ya wanawake tu. Aidha, imebainika kuwa utawala wa mfumo wa kuumeni katika jamii nyingi umekuwa ukitiwa nguvu na asasi ya dini. Hata hivyo mabadiliko yanadhihirika ambapo sasa mwanamke anaonekana kutawala hata katika familia.

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA

### 1.8.0 Historia fupi ya nadharia ya uhalisia

Katikati ya karne ya kumi na tisa huko ulaya, nguvu za mapinduzi ya kisiasa zilikuwa zimeanza kulegea. Mapinduzi ya kiviwanda nayo yalikuwa yamefikia kilele chake. Ulaya ilikuwa imeendelea sana kiteknolojia. Wanajamii walianza kukabiliana na matatizo yanayohusiana na miji inayopanuka harakaharaka. Tabaka la makabwela lilizuka. Uyakinifu wa hali ya binadamu ulithaminiwa sana. Huu ndio wakati ambapo Karl Marx alianza kuzungumzia jamii kisayansi huku akiagua yakwamba mapinduzi ya makabwela yangetokea baadaye, kama hatima ya historia.

### 1.8.1 Nadharia ya uhalisia katika mawanda ya fasihi

Katika mawanda ya fasihi, uhalisia ulitokana na matatizo kama vile ya kisiasa na kiuchumi yaliyokuwa yakiwakabili watu. Matatizo hayo yaliwafanya wanasanaa kuutuhumu ulimbwende. Matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Katika mwanzo wa karne ya kumi na tisa, Mfaransa Gustave Flaubert, mmojawapo wa waanzilishi wa uhalisia, aliupinga ulimbwende kwa kusema kuwa mtu hufikiria kwa kichwa wala si moyo wake (Wafula na Njogu, 2007). Ulimbwende ulikuwa unashughulikia mambo ya kidhahania ilhali wakati huo wa mapinduzi ya kiviwanda, matatizo ya watu yalikuwa ya kihalisia mfano tishio la ukosefu wa kazi kutokana na matumizi ya teknolojia katika viwanda.

Nadharia ya uhalisia inajihusisha na vitu thabiti vinavyohisika na mishipa ya fahamu ya binadamu. Kwenye fasihi, uhalisia unaonyesha uwezo wa kuchora au kusawiri hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Kando na Gustave, waandishi wengine wanaohusishwa na tapo hili la uhalisia ni Honore de Balzac na Emile Zola. Baadaye nadharia hii

ilisambaa kule Uingereza, Urusi na Marekani (Lawall na Maynard, 1984; Kearns,1996; Morris, 2003). Tapo hili la uhalisia liliwekewa misingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kiitwacho *Aesthetics*. Alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka (Wafula na Njogu, 2007).

Blunden (1976) katika kuangazia waliyosema Karl Marx na Engels kuhusu fasihi na sanaa, anasema kuwa wawili hawa walikuwa na maarifa mengi kuhusu sanaa na fasihi. Walipenda sana fasihi, nyimbo na uchoraji. Katika ujana wao, waliandika ushairi. Aidha, walizijua vyema kazi za wanafasihi kwa mfano Dickens, Balzac na wengine. Ingawa hawakuacha kazi za kimsingi katika sanaa, maoni yao kuhusu uwanja huu yakijumlishwa yana umuhimu mkubwa.

Kulingana na Blunden, Marx na Engels walifafanua umbo la sanaa na hatua zake za maendeleo na dhima yake katika jamii. Walieleza kuwa sanaa ni njia mojawapo ya utambuzi wa kijamii hivyo, sababu za mabadiliko ya sanaa zinafaa kuchunguzwa kupitia kwa uwepo wa wanadamu katika jamii. Katika kuchunguza maendeleo na ukuaji katika sanaa na ulimwengu wa mali na pia historia ya jamii, Wanaumaksi walitambua kuwa aina za sanaa na kilichomo kwenye sanaa hizo kilikua na kubadilika kulingana na sheria maalum, ukuaji wa ulimwengu wa mali na ukuaji wa jamii ya mwanadamu. Kila kipindi cha historia kina viwango vyake vya ujumi na huibua kazi za sanaa zinazooana na mambo katika kipindi hicho.

Kuhusu usawiri wa kihalisia, walisisitiza kuwa huu si uigaji tu wa mambo halisi bali ni njia mwafaka ya kupenya na kumulika hali mahususi katika jamii. Jambo hili ni muhimu katika kuweka wazi sifa kamili za hali fulani katika kipindi mahususi cha historia. Walilienzi na kulithamini sana jambo hili katika kazi za waandishi wa kiuhalisia kama vile Balzac.

Wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia hii waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo kwani fasihi ni kioo cha jamii. Hata hivyo, katika kuelezea ukweli huu mwandishi huteua mambo atakayosema. Wakati mwingine, yeye hutumia kejeli na udamisi ili kusuta maovu ya kijamii.

Ntarangwi (2004) anaeleza ya kwamba nadharia ya uhalisia katika upana humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Ilizuka kwa lengo la kupinga ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaozingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajriba. Vile vile, Wanauhalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha na malighafi ya kuelezea maisha ya kawaida ya kadri na ya kila siku. Hivyo basi, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya Mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi. Hivyo basi, hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii zapaswa kudhihirisha hali hiyo. Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia huonyesha namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyozingatia na wahusika anaosawiri. Yeye hutizama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum.

Maoni ya Scheidenhelm (2007) ni kuwa uhalisia hujikita katika matukio ya wakati na kipindi maalum na kuangazia matendo ya watu na athari za matendo hayo. Wanauhalisia huzingatia athari za kazi yao kwa wasomaji wao na maisha yao. Uhalisia haujaathiri tu taasisi na nyakati muhimu katika historia ya fasihi, bali pia umekuwa msingi thabiti wa fasihi nzima (Villanueva, 1997).

Baada ya Snow (1968) kutafiti kuhusu waandishi nane wa riwaya waliotumia uhalisia wakiwemo Honore de Balzac, Leo Tolstoy na Gustave Flaubert; aligundua kuwa kazi zilizochapishwa nyakati hizo za karne ya 19 zilijikita kwenye usawiri wa maisha fiche ya mijini mfano uhalifu. Hivyo kazi hizo zilikuwa na uhalisia kwani zilionyesha wazi uhalifu uliokuwa ukitendeka mijini.

Kulingana na Wamitila (2002), uhalisia ni mojawapo wa matapo maarufu katika ulimwengu wa fasihi na lenye athari kubwa sana. Dhana 'uhalisia' hutumiwa kwa maana mbili kuu. Kwanza ni kuelezea tapo la kipindi maalum cha kihistoria katika fasihi za ulaya. Pili, ni kwa maana ya mtazamo au tapo la kifasihi ambapo kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Basi, kazi zinazoangaliwa kama za kihalisia zinatarajiwa kuwa kama kisio la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Mtazamo huu unaweka mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii.

Larkin (1997) anasema kuwa wanauhalisia waliamini kuwa madhumuni ya kazi ya fasihi ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba ulimwengu unaoumbwa na kazi ya fasihi huwa na ukweli halisi wa wakati wake. Nadharia hii husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake. Yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi. Mwanasanaa katika misingi ya kihalisia anapaswa kuelewa ulimwengu wake kama kitu changamani na kinachobadilika.

Nadharia hii ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi ya sanaa na mtazamo wa msanii kuhusu mazingira anamojipata, (Lukacs, 1972)

Hart (2003) katika kuangazia nadharia ya uhalisiaajabu huko Amerika, anasema kuwa kazi za waandishi kama Marquez na Rulfo zimesawiri uhalisia kama ulivyo hasa lakini kwa kujumuisha

vipengele vya kimazingaombwe. Wanachunga uhalisia kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengee vya kifantasia na kindoto na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya. Ukweli huu pia unadhihirika katika riwaya ya *Dunia Yao* ya Said A. Mohamed ambapo ametumia mtindo wa uhalisiaajabu kuangazia mambo mengi sana ya uhalisia.

Kutokana na maelezo hayo yote ni wazi kuwa nadharia ya uhalisia itakuwa mwafaka katika kuchunguza mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume kupitia vipindi tofauti vya kihistoria na sababu ya mabadiliko hayo katika riwaya teule za Said. Hii ni kwa sababu matukio na mabadiliko halisi katika mazingira ya mwandishi hujidhihirika katika kazi yake.

Nadharia ya uhalisia ina mihimili ifuatayo itakayotumiwa kuongoza utafiti huu:

a) Ina mashiko katika hali halisi yaani hali zote za maisha ya jamii huelezwa jinsi zinavyoonekana wala sivyo zinavyofikiriwa kuwa. Uhalisia huu unaweza kubadilika wakati wowote. Aidha, inapinga dhidi ya mtazamo wa kijonzi juu ya maisha. Basi msomaji anafaa aweze kusafiri moja kwa moja na mwandishi kwa kuona kuwa yanayoelezwa yana uthabiti katika jamii. Hivyo, mhimili huu utatufaa katika kuchunguza mabadiliko ya nafasi na mitazamo ya wahusika wanaume kutokana na mabadiliko halisi katika jamii ya mwandishi Said.
b) Inaonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao. Aidha lugha wanayotumia ni ile ambayo msomaji anakumbana nayo. Mhimili huu utafaa katika kuona namna ambavyo wahusika wanaume katika riwaya teule wanaaafikiana na wanaume katika maisha halisi. Vile vile, jinsi mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule yanawiana na hali halisi katika jamii ya

msomaji. Pia mwandishi huathiriwa kisaikolojia kwa sababu ya matukio katika mazingira yake na huamua kusawiri wahusika wake kwa namna fulani ili kuondoa hisia hasi moyoni huku akiwasuta wenye kutekeleza uovu.

c) Mielekeo ya jamii haipingani na historia ya wakati wake. Hivyo historia ya jamii yoyote ile husawiri mwelekeo wake kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii ikiwemo fasihi. Mawazo haya ni muhimu katika utafiti huu kwani yatasaidia kueleza sababu ya kubadilika kwa nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume. Pia yatasaidia kuchunguza athari za mabadiliko hayo.

d) Kuna matumizi ya udamisi (vichekesho) na kejeli ili kupunguza ukali katika kusuta uovu. Kwa kutumia mbinu hizi, mwandishi hutumia wahusika wake kuwasilisha maudhui mazito ambayo hayangesemwa wazi wazi kwa sababu pengine yanaudhi. Kwa njia hii mwandishi huchochea jamii kubadili mienendo yake mibaya

e) Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Yeye huchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika kipindi fulani cha historia na namna ambavyo mabadiliko hayo husababisha hali mbali mbali.

Katika utafiti huu, tutajaribu kuoanisha malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia hii ya uhalisia.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Katika sehemu hii, vipengele vya muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, mbinu za usampulishaji, ukusanyaji na uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo vimejadiliwa.

### 1.9.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti na kuwasilishwa kimaelezo.

### 1.9.2 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambapo mtafiti alisoma kwa kina riwaya teule, vitabu, makala na machapisho.

### 1.9.3 Uteuzi wa sampuli

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa njia ya kimaksudi. Riwaya zilizotumiwa ni *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006) za Said A. Mohamed. Wahusika walioteuliwa kutoka kwa riwaya hizo mbili ni wale waliodhihirisha mabadiliko yanayoangaziwa na madhumuni ya utafiti huu. Katika kila riwaya wahusika waliteuliwa kulingana na jinsia ya kiume na nafasi zao katika riwaya.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa riwaya mbili za Kiswahili za Said A. Mohamed : *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006). Mtafiti alivisoma vitabu hivi na kuyatenga kwa kuyaandika mambo yote muhimu kwa utafiti huu, katika daftari. Mambo yaliyotengwa ni pamoja na nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume pamoja na mabadiliko yaliyojitokeza kuhusiana na suala hili. Aidha, vitabu vinginevyo, makala, tasnifu na machapisho mengine yenye ukuruba na kazi hii yalisomwa kwa upana. Vile vile, vitabu na makala yaliyoangazia nadharia ya uhalisia na historia ya mwandishi yalisomwa kwa undani. Kando na maktaba, usomaji wa tafiti,

vitabu na makala zinazohusiana na mada ya utafiti huu na hata nadharia yalisomwa kwenye mtandao.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa data

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kupanga data kwenye makundi kuzingatia mahusiano, ruwaza na mikondo inayopatikana ndani yake kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia iliyotumiwa. Hivyo, data kuhusu mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume, sababu za mabadiliko hayo na athari yake zilibainishwa na kuwekwa kando kando.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo

Baada ya kuchanganua data, matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kutumia lugha nathari. Maelezo haya yalizingatia malengo ya utafiti ambayo yalionyesha mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule, sababu za mabadilko hayo na athari zake katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui. Aidha, tulielekezwa na mihimili ya nadharia ya utafiti huu. Maelezo hayo ndiyo yamejenga sura tano za tasnifu hii.

# SURA YA PILI

## MABADILIKO YA NAFASI NA MTAZAMO WA WAHUSIKA WANAUME KATIKA RIWAYA TEULE

### 2.0 Utangulizi

Katika kila jamii huwa kuna nafasi au majukumu ambayo kila mtu anatarajiwa kutekeleza hasa kulingana na jinsia yake (Blackstone, 2003). Jamii nyingi za Afrika zimejikita katika mfumo wa kuumeni ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanamume katika nyanja zote za maisha. Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume yanadhihirika wazi kwa kulinganisha riwaya ya *Utengano* na ya *Dunia Yao*.

### 2.1 Mabadiliko ya nafasi

Nafasi ni jukumu au matumizi ambayo mtu au kifaa huwa nayo au hutarajiwa kuwa nayo (Kamusi ya Cambridge, 2008). Hivyo katika sehemu hii, nafasi ni jukumu alilonalo mtu au analotarajiwa kutekeleza katika kundi, jamii au uhusiano fulani.

#### 2.1.1 Mtafuta riziki

Mhusika mkuu wa kiume katika riwaya ya *Utengano* ni Bwana Maksuudi Kambe. Ana mke kwa jina Tamima na watoto watatu, Mussa, Maimuna na kitoto kingine kichanga. Bwana Maksuudi ndiye mwenye kufanya kazi ili kupata riziki. Yeye ni mkurugenzi wa shirika la Bima la Taifa na pia ananuia kuwania ubunge. Mkewe Bi. Tamima hafanyi kazi bali anaishi ndani ya kasri lililo na watumishi wengi. Hata hivyo, katika riwaya ya *Dunia Yao,* mabadiliko yanadhihirika kwa kumzingatia mhusika mkuu wa kiume Ndi-. Huyu ana mke kwa jina Bi. M na watoto sita, watatu wa kike kwa majina Mtima, Yungi na Kilua na watatu wa kiume wanaoitwa Dubwa, Bori na

Jitu. Bi. M ndiye mtafuta riziki katika familia hii. Yeye ana biashara ya kuuza vyakula ofisini. Anamweleza mumewe:

> Nakuletea chakula hiki. Nimekichuma kwa jasho langu na kukipika mwenyewe. Kama Nakuletea nilivyokwisha kukueleza, siku hizi nafanya biashara ya kuuza vyakula ofisini (Uk.23).

Baada ya kauli hii Ndi- anatuonyesha mawazo yake kuhusu Bi. M kutafuta riziki:

> Ningejuaje? Ningeweza kuchanganua vipi na kujua zipi nguvu za Bi. M na zipi za ukahaba wa Yungi? Na hata ningejua, bado maumivu ni maumivu. Sikutaka Bi. M atoke kutafuta riziki. Jukumu la kutafuta riziki lilikuwa langu. Ndivyo udume wa jamii hii ulivyoshikilia (Uk.23).

Kutokana na dondoo hizo inadhihirika wazi kuwa nafasi ya mwanamume ya kutafutia familia yake riziki imebadilika katika karne ya ishirini na moja. Sasa wanawake pia hutekeleza jukumu hilo iwapo mume ameshindwa au amepoteza kazi aliyokuwa nayo. Kwa upande mwingine, kutokana na utaratibu wa mfumo wa kuumeni kuwa kutafuta riziki ni kazi ya mume pekee; mwanamume anaonekana kuathirika hasa kisaikolojia. Kutokubali mabadiliko haya kunamfanya amuwazie mwanamke mabaya kwa kuamini kuwa mwanamke ameshiriki ukahaba ili alete riziki nyumbani. Mwanzoni, haamini kuwa mwanamke anaweza kufanya kazi yoyote halali na ya heshima ili apate riziki. Haoni ni vipi mwanamke anaweza kutekeleza jukumu ambalo tangu zamani ni la mume. Mume ndiye anafaa kuajiriwa au kufanya biashara ili apate pesa za kununua chakula na mavazi, kulipa karo na kugharamia mahitaji yote ya mke wake na watoto.

Jambo hilo la mwanamume kutoamini kuwa sasa mwanamke anaweza kufanya kazi kama mwanamume na kuleta riziki nyumbani linaendelea kushadidiwa kupitia kwa maneno ya rafiki ya Ndi- kwa jina Sakarati anayeongea kumrejelea mkewe. Anasema :

> Nitawezaje kuendelea hivi ? Nitawezaje kumwachia yule mwanamke atoke nje kutamba na ulimwengu huu mgumu wenye kila tashwishi za kishetani ? Iweje kuwa yeye awe mchumi ? Vipi achukue nafasi yangu ? (Uk. 51)

Kwa maoni ya mtafiti, majukumu ya kiuana yamebadilika sana katika karne ya ishirini na moja. Wanawake wameendelea kielimu na kiuchumi na hivyo wanaweza kuchangia katika kutafutia famila zao riziki.

### 2.1.2 Mtunga sheria na mdhibiti familia

Bw. Maksuudi katika riwaya ya *Utengano* anasawiriwa kama kiongozi katika familia yake. Ndiye anayetunga sheria zinazofaa kufuatwa nyumbani mwake. Kwa namna hii, aliidhibiti familia yake na wote kwenye kasri wakiwemo Bi. Tamima, watoto na hata watumishi wao. Yeyote anayekiuka sheria za Bw. Maksuudi anaadhibiwa vikali na bwana huyu. Hakuna anayefanya jambo lolote analotaka. Hakukuwa na uhuru huo. Aidha, Bwana Maksuudi amewatawisha Bi. Tamima na Maimuna hivi kwamba hawafai kutoka nje ya kasri bila ruhusa yake. Hata masomo yake Maimuna aliyapata akiwa ndani ya kasri hilo. Mwandishi anasema :

> Jumba la Bwana Maksuudi tuliite 'Kasri la Watawa'. Ni kasri kwa kimo chake, heba na uzuri uliostahili. Na ni la watawa, kwa sababu ya kukimwa kwa waliomo humo, mbali ya mwenyewe Bwana Maksuudi aliyejiwekea kutoka nje kwa kazi tu au pale alipokuwa na shughuli muhimu ya kibinafsi iliyohitaji usimamizi wake. Zaidi, wale watumishi wake wanaoruhusiwa kuingia na kutoka. Waliobaki walikuwa watawa. Na hawa hasa ni wawili, Bi Tamima, mkewe na Maimuna, bintiye (Uk.19).

Inadhihirika kuwa familia zilikuwa chini ya uongozi wa mwanamume kulingana na mfumo wa kuumeni. Kando na kutafuta riziki, mwanamume ndiye alitunga sheria na kumdhibiti kila mtu katika familia. Kwa maoni ya mtafiti, jamii ilimtarajia mume ahakikishe kuwa maadili mema yamefuatwa na mkewe na watoto wote. Maadili haya yalikuwa ni yale yaliyokubalika katika

jamii kwa mfano heshima ya watoto kwa wakubwa, unyenyekevu wa mke kwa mume wake na kadhalika. Mwanamume alikuwa amepewa mamlaka mengi juu ya watoto, wafanyikazi na hata mke wake. Wanaume wengine hata walizidisha mamlaka yao na kuwatawisha watoto wa kike na pia wake zao. Mwanamke alinyenyekea na kuishi kwa woga mwingi kwani wakati mwingine alipigwa na mumewe hata kwa makosa yasiyokuwa yake. Kwa upande mwingine, mume alikuwa na uhuru wa kufanya lolote alilotaka na wengine hata walifanya lile lisilolingana na maadili tarajiwa ya jamii.

Bi Tamima anaposhikwa na uchungu wa kujifungua, bintiye Maimuna anajaribu kumshauri akubali kupelekwa hospitali akajifungulie huko au si hivyo akaitiwe daktari. Lakini Bi. Tamima anakataa katakata mashauri yote mawili. Anasema:

> Mm-u, mm-u…babaako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake, na humu asiingie mtu ila kwa ruhusa yake (Uk. 20).

Kutokana na nafasi ya mwanamume ya kutunga sheria na kudhibiti familia, wanawake wengi waliogopa hata kuchukua hatua muhimu kuhusu maisha yao. Kwa namna hiyo, walionekana kuwa tayari kuhatarisha maisha yao ilimradi wasitende kinyume na sheria za waume wao.

Aidha, watoto walipofanya makosa wanaume waliwaadhibu vikali ili wasirudie makosa hayo. Haya yalionekana kupitia kwa kisa cha Bwana Maksuudi kumwadhibu Mussa vibaya sana nusura amuue kwa sababu ya kushiriki uasherati na mwanamke aliyeitwa Kazija. Tunaelezwa:

> Mussa alijaribu kuinuka, lakini alihisi kizunguzungu. Tahamaki Bwana Maksuudi amemkalia juu ya kifua na vidole vyake vya mikono vimechopea shingoni pake. Mussa alianza kuuhisi mdidimizo. Pumzi zikaanza kumwia chache. Zikazidi kuwa haba kila vidole vilivyozidi kuchopea. Mussa alishika mikono ya babake imara. Alizuia kwa nguvu, bali baba mtu alizidi kukaba. Mussa alikoroma, kipovu kikamtoka (Uk. 14-15).

Kinyume na hayo, katika riwaya ya *Dunia yao* mabadiliko makubwa yanadhihirika kuhusiana na jambo hili. Ndi- anayapoteza mamlaka yote ya kuiongoza na hata kuidhibiti familia yake. Kila mmoja anafanya analotaka na kwenda anakotaka bila wasiwasi wowote.

> …Jumapili nyumba ilijaa zogo na pirikapirika na ingia toka na vifijo na shangwe za wenye nyumba na wageni wao. Ule utulivu niliouweka miaka yote katika nyumba hii, sasa haukuwemo tena (Uk. 89).

Kutokana na mamlaka aliyopewa mwanamume katika jamii, inatarajiwa kuwa uwepo wa baba katika familia uibue hisia za utulivu, unyenyekevu, utaratibu na hata heshima ya watoto kwa wazazi wao. Hatutarajii kumpata mtoto akileta wageni pale nyumbani kwa wazazi wake bila ruhusa. Hata hivyo, katika karne ya ishirini na moja, mabadiliko yamezuka. Watoto wengi hawawaheshimu wakubwa wao hata kidogo. Wao wanayafanya wapendayo na kuonekana kujitawala kabisa. Wanavuka mipaka kwa kukosea nyumba za wazazi wao heshima kwa kuwaleta rafiki zao pale nyumbani bila ruhusa ya wazazi. Zaidi ya hayo, wanajivinjari kwa kelele bila kujali uwepo wa wazazi.

Aidha katika kuendelea kutuonyesha jinsi watoto wanafanya wapendavyo licha ya kuwa bado wanaishi kwa wazazi wao mwandishi anatueleza jinsi Yungi, bintiye Ndi-, anarudi nyumbani akiwa amechelewa na yu mlevi.

> Yapata saa tisa na nusu za alfajiri aliporudi, jimbi la kwanza lilipolia. Aligonga mlango, huku akikiendeleza kicheko alichokuja nacho. Lile kundi lake la suhuba lilikuwa limeshatoweka na gari. Mamake ndiye aliyemfungulia mlango baada ya kugonga. Akaingia ndani na uchangamfu na kicheko cha kilevi (Uk.24).

Wazazi wa kiume katika karne hii wanaonekana kushindwa kabisa kuwadhibiti watoto wao. Aidha, huwa hawaadhibu watoto wakifanya makosa. Wamebadilika kiasi cha kutowakanya watoto wao wa kike na hata wale wa kiume kurejea nyumbani usiku. Fauka ya hayo,

hawawaadhibu watoto wanapojiingiza katika ulevi wa aina yoyote. Wao hunyamaza tu hivyo watoto wanazorota kimaadili.

Yungi anaporudi nyumbani akiwa mlevi, mwandishi anasema kuwa anaanza kupayuka ovyo mbele ya Ndi- na mkewe. Anamweleza babake kuwa:

> Lazima uukubali ukweli. Wakati umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Pia huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume (Uk.25).

La ajabu ni kuwa hatumwoni Ndi- akimkanya au kumwonya anyamaze. Bi. M ndiye anamwonya anyamaze. Ndi- anasema:

> Nilitaka niinuke nifanye kitu, hata sikujua kitu gani, lakini sikuweza. Nilitaka kusema nijitetee. Nijibu kitu chochote japo kisicho maana. Nilitaka kuchukua hatua nyingine ya kumnusuru Yungi kwa maneno au vitendo kwa kitendo. Lakini maneno yepi? Kitendo gani ? Maneno na vitendo nimeviisha kwa muda wa miaka kumi na tisa ya umri wake…Hatamu za maisha yake anazo mwenyewe sasa (Uk.25).

Haya ni mabadiliko ambayo yalikuwa nadra kuyasikia katika karne iliyopita. Mwanamke sasa huonekana ndiye anajaribu kuidhibiti hali kwa kuwaadhibu watoto vikali pindi wanapokosa.

Zaidi ya hayo, wakati mmoja Ndi- alipomwona bintiye Yungi akiwa amekamatwa na bwana mmoja, hawaambii lolote wala hamkanyi. Anaingia chumbani mwake mbio na kuufunga mlango.

> Ikadhihiri mandhari ambayo nisingetaka inifumanie maisha yangu. Alikuwa Yungi nywele timtim na khanga moja kifuani kajijambika. Katiwa ngosho kiunoni na bwana mmoja aliyeshiba maziwa ya mamake. Wanakwenda chooni kwa shangwe, vifijo na furaha. Niliufunga mlango kwa kasi ya ajabu. Kama kupwesa, nikajikuta ndani, nahema kama nilimaliza mbio za masafa marefu. Ilikuwa siku yangu yamwanzo kumwona Yungi namna ile na kujua kwamba mambo yamefikia hadi hiyo (Uk. 77).

Uwezo na mamlaka ya mwanamume juu ya watoto wa kike unaonekana kuisha kwani hata watoto hao wakijiingiza kaika uasherati mzazi wa kiume hasemi lolote. Ni kana kwamba wameamua kuwaacha watoto wajitawale hivyo kujiamulia mienendo watakayofuata. La mno ni kuwa, baadhi ya wanaume wanajificha badala ya kuwazungumzia binti zao au kuwaamuru wazazi wa kike wawazungumzie na kuwakanya wasichana hao. Ni dhihirisho tosha kuwa nafasi aliyokuwa nayo mwanamume ya kudhibiti familia yake imebadilika kabisa. Tamaduni na mila za Kiafrika hazifuatwi tena. Wazazi wa kiume wamekuwa kama bubu au vipofu. Hata wakiona watoto wao wakitenda maovu, hawatekelezi jukumu la mzazi la kumwadhibu na kumrekebisha mtoto.

Wakati ambapo Jitu na Bori walikuwa wakipigana mle ukumbini, Ndi- alipofika alimkuta Bi. M amemkunja shati Jitu anamzaba vibao. Bi. M anawaeleza:

> Msidhani nyumba hii imepoteza mchunga, mkafikiri mnaweza kutututurisha roho zetu. Mmehamisha kila kitu. Sasa mnataka kuhamisha roho zetu. Pigana na mimi kama kweli wewe mwanamume. Na wewe Bori umempiga mwenzako na kumdhuru namna hii! Na wewe kigego cha mwanamke unashangiria vita, unaviweza? (Uk. 135-6).

Hata ndugu wakipigana wenyewe kwa wenyewe, wazazi wa kiume hawafanyi lolote. Mambo yanapokuwa mabaya zaidi, tunawaona wazazi wa kike wakichukua hatua ya kurejesha amani nyumbani kwa kukomesha fujo.

Vile vile, wakati Mtima bintiye Ndi- aliamua kugura na kwenda Uingereza, licha ya umri wake mdogo, hatumwoni babake akimwuliza maswali yoyote kuhusiana na jambo hili. Baadaye Ndi- anasema:

> Aaaa, kauli hii ilikuja kunishangaza na kunibeza baadaye. *Ilikuwaje kwanza nikazibika fikra namna ile? Kwa nini nilikubali kirahisi Mtima aondoke? Kwa nini nilitoa uamuzi ule usio na busara wala misingi ya hofu na ubaba? Mtoto mwanagenzi aliye peke yake katika dunia ya ujalaana, balaa na ushetani!* (Uk. 10)

Mzazi wa kiume kama kiongozi katika familia yake alitarajiwa kuyaelekeza maisha ya watoto wake hasa watoto wa kike ambao bado hawajaolewa. Hata hivyo, katika karne ya ishirini na moja, watoto wanajiamulia mambo yote hata yale tungetarajia kusikia wakipewa ushauri na wazazi. Licha ya umri mdogo wa baadhi yao, watoto wanaondoka nyumbani na kusafiri nchi za mbali kuenda kutafuta kazi au kuishi peke yao. La kustaajabisha ni kuwa, hatuwaoni kina baba zao wakiwauliza lolote au kujaribu kuwakataza au kuwashauri kuhusiana na uamuzi wao wa kuondoka. Baadaye wanaume hawa wanakuja kujutia uamuzi wao.

### 2.1.3 Mtafuta suluhisho la matatizo na asiyekata tamaa

Katika riwaya ya *Utengano*, tatizo lolote linapotokea katika familia yake, Bwana Maksuudi anajaribu kukabiliana nalo kwa namna yoyote ile. Hakati tamaa kwa haraka. Kwa mfano, anapomfukuza mkewe Bi. Tamima na hatimaye kuisambaratisha aila yake, anagundua kosa lake na kufanya juu chini ili kuwatafuta. Anamwandikia Bi. Tamima barua moja baada ya nyingine akimwomba msamaha na akimrai arudi licha ya Bi. Tamima kukataa kuzijibu. Kando na hilo, Maksuudi agunduapo kuwa bintiye Maimuna alipotoroka alikwenda kuwa mwimbaji wa nataki katika hoteli ya Rumbalola huko Bobea; anasaidiwa na dereva wake kwa jina Rashidi kupanga safari ili kwenda kumrai Maimuna arudi nyumbani. Hata hivyo hafanikiwi. Maimuna alitorokea nyuma ya jukwaa. Naye Maksuudi alivamiwa na watu na kupigwa vibaya kwa kuwaharibia raha zao. Hafi moyo ila bado Bwana Maksuudi anapanga safari nyingine ya kwenda katika klabu ya Biti Sururu kule Bobea anamofanya kazi Maimuna ili kujaribu kumrai arudi nyumbani. Hata gari

lao linapofika mahali ambapo halingepita, inawabidi watembee. Licha ya Bwana Maksuudi kuwa na kiharusi, tunamwona akijikaza kabisa. Mwandishi anaeleza:

> Lakini Maksuudi aliendeshwa na ari na haja, ndani akiwa na shajiisho lililofanya mwili wake usihisi maumivu…. Mara mbili Maksuudi alichopea. Na mara moja mguu wake mgonjwa uliingia shimoni na kuchunikachunika. Bali hakujali. Alikokota mguu wake kwa dhamiri zaidi (Uk. 131-132).

Pia mwandishi anatueleza kuhusu mwanamume mwingine kwa jina la Kabi. Licha ya kuupoteza mguu wake wa kushoto hapo zamani, hatumwoni akikata tamaa maishani. Anaamka alfajiri saa kumi na kujishughulisha na uvuvi wa samaki ili ajikimu kimaisha. Baada ya kuoa na kuhamia kijiji cha Hitama anaendelea na bidii katika ukulima.

> …naye Kabi mwenye mguu mmoja aliwashangaza majirani zake jinsi alivyokuwa na juhudi ya kazi (Uk. 172).

Mifano hiyo inadhihirisha kuwa mwanamume anatarajiwa awe mkakamavu licha ya changamoto zinazomkumba. Hata zikiwa ni za kimwili kwa mfano kupooza, mwanamume anatarajiwa kujikaza na kujizatiti ili afanikiwe katika jambo lolote lile. Hatarajiwi kufa moyo au kukata tamaa upesi. Anafaa kuwa kielelezo cha mwanamume kamili asiyejihurumia kwa sababu ya shida zinazomkabili.

Kwa upande mwingine, mwanamume katika riwaya ya *Dunia Yao* amesawiriwa kama kiumbe cha kukata tamaa upesi sana. Kwa mfano, badala ya kutafuta njia mbadala ya kujiendeleza kimaisha baada ya jambo baya kutendeka, wanaume wanakufa moyo na kuomboleza daima. Hatuoni wakichukua hatua za kukabiliana na matatizo mbalimbali au changamoto zinazowakumba. Baada ya kufutwa kazi katika ofisi ya serikali, Ndi- ananywea kabisa na

kujifungia chumbani hadi watu wanamdhania kuwa mwendawazimu. Anabadilika na kuwa mnyamavu kiasi cha kutozungumza na yeyote katika aila yake hata Kilua anayempenda babake sana. Kilua anamweleza:

> Hutaki kusema na mama, na dada Yungi, na kaka Bori na kaka Jitu na kaka Dubwa.... husemi na yeyote (Uk. 59).

Aidha, wakati mwingine Ndi- anapoamua kwenda barazani, anahakikisha kurudi wakati kila mtu ameshalala. Anasema:

> Kwa hakika siku hizi huchelewa kurudi kwa fedheha ya kushindwa kuikimu nyumba yangu. Huona nibaki nje na kuingia ndani kila mtu anapokuwa keshalala, ili kukimbia nyuso zao kuniona (Uk.19).

Ndi- anapokuwa katika baraza la wazee, rafikiye Sakarati ambaye pia hakuwa na kazi anawasili. Anaomboleza hali yake kwa kilio hasa kutokana na mkewe kuwa ndiye mtafuta riziki siku hizi. Silima, rafiki yake Sakarati tokea utotoni anafika na kumweleza:

> Mtazame analia. Baradhuli nini wewe? Nyamaza. Jikaze kidume. Ndio ulimwengu. Unamlilia nani asiye na mzigo wake? Pengine mkubwa zaidi kuliko wako! Sakarati alizidi kulia tu. Sasa kwa nguvu zaidi. Silima alikuja kumwekea mkono wa bega. Akawa anamsihi kwa utaratibu sasa. (Uk. 52)

Ni dhahiri kuwa wanaume katika karne ya ishirini na moja wamebadilika sana. Inashangaza kuona jinsi wanavyokata tamaa upesi eti kwa sababu ya kukumbwa na changamoto kama vile kufutwa kazi. Badala ya kujikaza kidume, tunawaona wengine wao wakilia hadharani na inabidi wabembelezwe kama watoto wadogo ili wanyamaze. Hawadhihirishi kamwe ukakamavu na ujasiri unaohusishwa na wanaume katika jamii nyingi. Fauka ya hayo, wanaume wa karne hii wanapopata matatizo, wanashindwa kabisa kuchukua japo hatua moja ili kuyatatua. Hatuwaoni wakitafuta suluhisho. Wengi wao wanatorokea shida zao kwa kujifungia vyumbani au hata

kujiingiza katika ulevi. Tungetarajia kuwa, mwanamume akipoteza au kufutwa kazi moja atafute nyingine. Ikiwa amefutwa kazi ya ofisi inatarajiwa atafute kazi katika ofisi nyingine au hata aanzishe biashara yoyote ile ili ajikimu au aikimu familia yake. Ni kinyume na matarajio yetu kuona mwanamume amekosa kujali, akajifungia chumbani na kutengana na wanadamu wengine eti kwa sababu amefutwa kazi. Kwa maoni ya mtafiti, Ndi- na Sakarati walifaa kutafuta au kuanzisha kazi nyingine ilimradi waweze kukimu familia zao. Kwa namna hii, watoto wao hawangewacha masomo yao kutokana na ukosefu wa karo. Hivyo, watoto hao hawangetaabika maishani kama ilivyodhihirika katika riwaya.

### 2.1.4 Mfanya kazi za nje bali si ndani ya nyumba

Katika riwaya ya *Utengano*, imedhihirika wazi kuwa mwanaume alitarajiwa na jamii kufanya kazi za nje ya nyumba kama vile kulima, kukwea minazi, udereva na kazi nyinginezo za kutafuta riziki. Kwa mfano, Rashidi alifanya kazi kama dereva wa Bwana Maksuudi naye Shoka mumewe Selume alikuwa kuli bandarini. Maksuudi na Zanga walikuwa viongozi wa kisiasa na walikuwa na ofisi zao. Wanaume wengine walifanya kazi ya kupanda minazi kwa mfano Mzee Mabruki aliyefanya kazi hiyo kwa miaka mingi. Naye mwanamke alitarajiwa kufanya kazi za nyumbani kama vile kulea watoto, kupika, kufagia nyumba, kuosha vyombo na kadhalika. Mussa katika ulevi wake alimuuliza Kazija yeye alikuwa nani na tunayaona mawazo ya Kazija kuhusu kazi za mwanamke;

> Mwanamke, mtumwa. Nani kasema utumwa umeondoka? Viumbe vya kupika na kupakua, kufua na kupiga pasi, kushika mimba na kuzaa, kuzaa, kuzaa, kuzaa kama panya…na kutawa na kutawishwa (Uk. 7).

Mabadiliko yanadhihirika wazi katika riwaya ya *Dunia Yao* ambapo Ndi- anafanya kazi za nyumbani wakati ambapo mkewe Bi. M anaenda kazi ya kuuza chakula ofisini ili wapate riziki naye bintiye Yungi amekwenda mkutanoni.

> Tokea kuzaliwa kile kitoto kipya, siku hizi Bi M mkewe, akigonga mlango, Ndi-huenda kuufungua. Na mara nyingi ilikuwa kuamshwa kusaidia kazi za nyumba: kufagia, kusafisha msalani, kufua nguo, kupiga pasi na bila ya shaka kubaki na Bisudi, kitoto chao kipya cha miezi mitatu.
>
> "Yungi amekwenda mkutanoni…Si unajua kwamba wanataka kuvunja nyumba za eneo letu hili lote kwa kujenga hoteli ya Wataliano? Yungi amechaguliwa kuwa kiongozi na kwa hivyo yumo mbioni, kukutana na wakaazi…Na mimi natoka kupeleka chakula maofisini…Ninakuletea Bisudi ukae naye. '' Bi. M alimjulisha Ndi- (Uk. 210)

Kinyume na ilivyokuwa miaka ya awali, mwanamume sasa anawachiwa watoto pale nyumbani ili awalee ilhali mwanamke amekwenda kazini nje. La mno ni kuwa, hata anawachiwa watoto wa umri wa miezi kadhaa ili awachunge naye mke aende kazini. Mwanamume anamruhusu mwanamke kushiriki masuala mengine ya ujenzi wa taifa kwa mfano biashara. Aidha, anawaruhusu hata watoto wa kike kujihusisha na maswala ya kisiasa kwa mfano kupigania haki za wananchi. Wanachaguliwa hata katika vyeo vya uongozi kinyume na miaka ya awali ambapo walikuwa wakipingwa vikali. Wanaume nao wanashiriki kazi za nyumbani kama vile kufagia, kufua nguo, kusafisha msalani, kupiga pasi na zaidi ya yote kuwa yaya. Haya ni mabadiliko makubwa sana yasiyofikirika kulingana na tamaduni na mila za Kiafrika zikiwemo sehemu za Unguja alimozaliwa mwandishi wa riwaya teule. Kazi kama hizo zilihusishwa na wanawake waliotarajiwa kubaki nyumbani nao wanaume waende kazini nje. Hata kama mume hakuenda kazini siku fulani, hakutarajiwa kusaidia kazi kama hizo kwani zilihusishwa na jinsia ya kike pekee kama alivyodhihirisha P'Bitek (1966:133):

> …mwanamke wa Afrika, mfagiaji, anakandika sakafu na kuta kwa samadi na

> udongo mweusi. Mpishi, yaya, huku mtoto amefungwa mgongoni, anatapika. Mwosha vyombo, anapanda, anapalilia, anavuna. Mtunza vifaa, mjenzi, kijakazi, lori, mkokoteni, punda. Mwanamke wa Afrika, ni nini usichokuwa.

Mfano huu ni ithibati tosha kuwa kazi za kinyumbani zilihusishwa na mwanamke. Ni mabadiliko yaliyoje kumwona mwanamume katika karne ya ishirini na moja akitekeleza kazi zizo hizo!

### 2.2 Mabadiliko ya mtazamo

Mtazamo ni namna ya kuangalia au kutazama kitu au mtu. Ni jinsi mtu anavyochukulia au kufikiria jambo. Yaani ni mawazo ya mtu juu ya jambo fulani (Kamusi ya TUKI, 2004)

#### 2.2.1 Mtazamo kuhusu uhuru wa mwanamke

Kwanza kabisa katika riwaya ya *Utengano*, mwanamume amemnyima mwanamke uhuru wa mambo mengi. Kwa mfano, mhusika mkuu Bwana Maksuudi amemnyima mkewe Bi Tamima na bintiye Maimuna uhuru wa kutoka nje. Aidha, hawawezi kujieleza au kutoa uamuzi wa mambo yanayowahusu. Katika kasri hili, Bwana Maksuudi ndiye mwamuzi wa mambo yote. Aidha, elimu ya watoto wa kike kwa mfano Maimuna ni ya ndani ya nyumba anamotawishwa hivyo hawafiki katika ngazi za juu za masomo mfano chuo kikuu.

Mussa kwenye ulevi wake katika chumba cha Kazija anaanza kuboboja kwa Kizungu. Kazija anamweleza:

> …usiniseme Kizungu miye. Si ndivyo mlivyotuweka? Tusisome. Tuwe wajinga. Mtutawale na kutuparamia maisha, au sivyo ? (Uk. 8) ...

Mwishoni mwa riwaya baada ya Maimuna kuolewa na Kabi, Maimuna alipokuwa akisoma gazeti, Kabi anamweleza:

> Maimuna wewe una fahamu nzuri na akili yako inafanya kazi vizuri zaidi kuliko mimi, lakini…(Uk.173)

Maimuna naye anamweleza Kabi:

> Lakini ni kosa la babangu…hata sijui angalinisomesha ndani ndani mpaka lini? (Uk. 173)

Bwana Maksuudi, babake Maimuna, alikuwa amemsomesha mwanawe wa kiume Mussa hadi chuo kikuu na baadaye akawa daktari kule Pumziko. Hata hivyo, anamwelimisha Maimuna ndani ya nyumba licha ya kuwa na fedha na uwezo.

Mabadiliko yanadhihirika katika riwaya ya *Dunia Yao* ambapo tunaona wanaume wakiithamini elimu ya watoto wa kike sawa na ile ya watoto wa kiume. Ndi- anawaelimisha wana wake na binti zake hadi pale alipofutwa kazi na kushindwa kuimudu karo. Ndi- anasema kuwa Dubwa, mwanawe, alifaulu vyema mitihani yake shuleni na chuoni. Alifika kiwango hicho kwani babake hakuwa amefutwa kazi. Katika muktadha mwingine, kwa hasira Yungi anamweleza babake Ndi:

> Hata ile elimu uliyoisimamia kidete na kunikandamiza nayo kwa maneno na vitendo ili nifaulu katika kila hatua yake, sasa imefaa nini ? Hizi ‘A’ nilizonazo katika shahada ya kidato cha sita zinasaidia nini? Mwaka wa saba huu sijapata kazi wala nafasi ya kuingia chuo kikuu kwa ukosefu wa malipo… (Uk. 105)

Ni wazi kuwa hapo awali wanaume hawakuuona umuhimu wowote katika elimu ya watoto wa kike. Kwa maoni ya mtafiti, kusomesha msichana sana kulionekana bure au njia ya kuharibu pesa kwani angeolewa na asalie tu pale nyumbani kuzaa, kulea na kufanya kazi za pale nyumbani. Kwa upande mwingine, katika karne ya ishirini na moja, wanaume wanaonekana kubadili mtazamo wao kuhusiana na suala hili. Wanaonekana kuwapa wanawake uhuru wao na

kujitahidi kuwasomesha binti zao hadi viwango vya juu kabisa. Aidha, wanawaruhusu kufanya kazi popote wapendapo hata ikiwa ni nchi za ng'ambo. Hawawaoni wanawake tena kama viumbe vya kufugwa nyumbani kama kuku. Wengi wao wanaithamini sana elimu ya watoto wa kike na kuwahimiza kwa maneno na vitendo wajikaze ili wafanikiwe. Mtafiti anaona kuwa kama Ndi- hangefutwa kazi angeendelea kuwasomesha watoto wake hadi ngazi za juu kwa mfano Yungi na wapate kazi za kumudu maisha yao.

Aidha, Ndi- anauheshimu uamuzi wa bintiye Mtima wa kutaka kwenda Uingereza. Baada ya kumruhusu Ndi- anawaza;

> Potelea pote na aende, ameshakuwa mkubwa wa kuiendesha nafsi yake ndani ya dunia yake (Uk. 10).

Ni wazi kuwa wanaume wamewapa wanawake uhuru wao hata wa kusafiri nchi za ng'ambo ili wakafute kazi. Mtazamo wao sasa ni kuwa mtoto wa kike akishafika umri fulani, anaweza kwenda kujiendeleza mahali kwingine. Hatuoni wanaume wakiwanyima uhuru au kujaribu kuwafuata walikoenda na kuwarejesha nyumbani.

### 2.2.2 Mtazamo kuhusu ukwasi na madaraka

Katika riwaya ya *Utengano*, mhusika mkuu Maksuudi anaamini katika kupata chochote atakacho kwa njia yoyote ile hata ikiwa ni kwa kuwakandamiza wengine. Anaamini katika kutumia unafiki, unyang'anyi na hata madaraka au cheo chake kupata atakacho. Jambo hili linamfanya afanye mambo ya kikatili kwa watu wanyonge katika jamii yake. Mwandishi anatueleza jinsi Maksuudi alipata shamba lake lililo katika kitaa kidogo cha Via.

> Kupatikana madaraka, Maksuudi alichaguliwa Mkuu wa Wilaya, na ilivyokuwa kitaa hiki kilikuwa katika wilaya yake, alirithi nyumba na shamba pia kwa mipango bila ya shaka, ambayo mpaka leo ilikuwa ni siri yake (Uk. 98-99).

Katika uwanja wa Uhuru, Bwana Maksuudi, Zanga na wanasiasa wengine wanasimama jukwaani kutoa hotuba za kuomba kura za ubunge. Wakati wa kuuliza maswali unapofika, hawara wa Maksuudi kwa jina Kazija anapasulia umma mbarika kuwahusu wawili hao (Maksuudi na Zanga) waliotaka kuchaguliwa tena.

> Wananchi wenzangu, haifai kuiacha fursa hii. Hawa mahaini walitupa nafasi tuwasubu na sisi tulinyamaza kimya. Nani asiyemjua Zanga hapa? Nani asiyejua hali aliyokuwa zamani? Leo mtazameni yeye nani…Ana magari matatu. Ana nyumba tatu…Kazini hapatikani ila na watu wakubwa kama yeye na kwake sasa hawaendi watu ovyo. Lugha yake ni ujeuri. Mkabala wake na watu ni wa majivuno na zaidi hana imani wala fikra kwa wale ambao wamemnyanyua. Na Maksuudi…Mbali na mali aliyojilimbikia, nyingine ya unyang'anyi kwa wake zake. Amemnyang'anya mkewe mmoja, Mwanasururu, mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo chake (Uk. 80-81).

Ikizingatiwa kuwa wanaume ndio walikuwa watafuta riziki, tunaona kuwa walikuwa wanafanya kazi kama vile za ukulima, udereva na hata kazi katika ofisi za serikali. Inabainika kuwa tamaa na ubinafsi mwingi wa wahusika wanaume uliwafanya wakose hata chembe ya utu ndani yao. Walikuwa tayari kutumia unafiki wa kidini, uwongo na ulaghai wa aina yoyote ile mradi wapate ukwasi na madaraka katika jamii. Wanashiriki hata biashara haramu bila woga wowote ili kuwa na ukwasi mwingi. Walijifanya wacha Mungu ili watu waamini na kuwapa vyeo mbalimbali.

Mabadiliko yanajitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* kupitia kwa mhusika mkuu Ndi-. Ana mtazamo hasi kuhusiana na tabia ya kutumia mbinu za kuwakandamiza wengine ili upate ukwasi na mali isiyo halali. Haya yanadhihirika kutokana na anayosema Ndi-:

> Sijawahi katika maisha yangu kutaka kukanyaga na kusagasaga watu kwa nguvu za kipawa changu. Jambo ambalo kila siku hutaka kuliepuka maishani mwangu mote. Wala sijawahi kuota kuwa na ukwasi au ujeuri, kiburi na kuvimbisha kichwa. Wazimu mkubwa usiokadirika duniani. Kuna nini katika mali na ukwasi? Kuna faida gani katika madaraka na nguvu? Na unapovimbisha kichwa mwishowe ni nini kama si kupasua watu

> na kupasuka mwenyewe. Nini zaidi kilichomo ndani ya haya yote kama si uharibifu wa nafsi yake mtu na nafsi za wengine? Lini atazuka tena Zulkarnein, mfalme aliyepewa na Mungu wake nguvu juu ya kila kitu na kila mtu, na bado akawa anaijua mipaka yake. Akawa anajua kumheshimu kila mtu! (Uk. 8-9)

Wanaume sasa wameonyesha kuchukizwa na tabia ya ubinafsi na ubepari. Kupitia kwa mhusika mkuu, tunaona wazi kuwa ni vyema wanadamu kuwa na utu. Zaidi ya hayo, tunagundua kuwa ni vyema kuwa na moyo wa kiasi ili ujue kuweka mipaka. Haifai kuukimbiza ukwasi na madaraka kama kipofu kwani mwishowe utaangamia wewe na pia kuwaangamiza wengine. Mtu akibahatika kupata cheo au madaraka yoyote maishani, hafai kuwa na kiburi na kuwadharau walio chini yake. Badala yake anafaa ajitoe mhanga kuwahudumia kwa uaminifu wa hali ya juu na kuwaletea maendeleo maishani. Kwa njia hiyo, watamheshimu na hata kumpa madaraka tena lakini akiwa ni mtu mwenye tamaa mwishowe ataizorotesha nchi na watu wote watataabika.

### 2.2.3 Mtazamo kuhusu kazi na malipo halali

Katika riwaya ya *Utengano*, Bwana Maksuudi alishiriki ufisadi badala ya kufanya kazi kwa njia inayostahili na kwa kudumisha uadilifu kama kiongozi. Katika uwanja wa Uhuru, Mzee Japu aliwaza moyoni;

> Maksuudi.aaa, alipokuwa Mkuu wa Wilaya, alikula pesa ngapi za mke wangu alipotaka kununua kiwanja cha kujengea nyumba. Sahihi yake tu Mkuu wa Wilaya aliiuza shilingi mia mbili (Uk. 78).

Hii ni tofauti kabisa na Ndi- katika *Dunia Yao* ambaye anasema kuwa kazi nzuri ni ile ambayo ni halali na yenye mapato halali kwa mfano kazi ya ualimu, uandishi wa sanaa na kadhalika. Fauka ya hayo, mtazamo wake ni kuwa mtu anafaa kutosheka na mshahara apatao kwa kazi yake bali si kuongozwa na ukorofi.

> Ilitosha kwangu kufanya kazi ya halali na kupata malipo ya halali. Na wakati ule malipo ya halali yaliweza kukimu maisha yangu na ukoo wangu na kusaza bakaa. Nilitaka tu kazi ya kutenda na kutendeka mimi mwenyewe…Kazi ya furaha kwangu na kwa wengine. Kazi ya manufaa kwa wote (Uk. 17).

Mtazamo wake kuhusu kazi ya utawala ni kuwa;

> Kazi ya utawala ni kazi ya ukorofi, kwangu na kwa wengine. Ilikuwa ni namna fulani ya uungumtu. Niliidharau kwa hivyo, ingawa katika daraja niliyokuwa, hasa wakati ule, ilikuwa na pesa nzuri na fursa ya kugeuza maisha ya mtu. Ilikuza kichwa cha mtu na kumfanya ahisi angeweza kugusa mbingu (Uk .17).

Kutokana na mifano hiyo inabainika kuwa, mtu anafaa kufanya kazi ya halali yenye kumpa malipo ya halali katika jamii. Pia mtu anafaa kuepuka kazi ambazo zitakandamiza wengine. Maadili mema kama vile utu, uwazi na kuridhika na ulichopata ni bora zaidi kuliko malipo yaliyopatwa kwa njia isiyo halali. Badala ya kushiriki uovu, ni bora zaidi mtu kuukemea. Ni wazi kuwa katika karne ya ishirini na moja kuna wanaume ambao wanaonea fahari uadilifu hasa kuhusiana na masuala ya pesa na vyeo. Hawako tayari kushiriki kazi zinazowafanya waonekana kama miungu wadogo huku wakiwanyanyasa. Kwao, inatosha kushiriki kazi halali yenye kuwaletea wao binafsi na wanajamii wengine heshima na manufaa. Iwapo kazi na vyeo walivyopewa vinahatarisha hayo mambo mawili, basi wanaonekana kuwa tayari kuviwacha vyeo na kazi hizo.

## 2.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeonyesha mabadiliko ya nafasi ya wahusika wanaume kama yalivyodhihirika katika riwaya teule. Imedhihirika wazi kuwa hapo awali, mwanamume ndiye alikuwa mtafuta riziki lakini sasa wanawake ndio wanaitafuta. Aidha, nafasi ya mwanamume ya kutunga sheria na kudhibiti familia, kuleta suluhisho la matatizo kwa kutokata tamaa na pia nafasi ya kufanya

kazi za nje ya nyumba imebadilika kwa kiasi kikubwa. Vile vile, mabadiliko ya mtazamo wa wanaume yameangaziwa. Kwa mfano, kuhusu uhuru wa mwanamke, ukwasi na madaraka na mwisho kufanya kazi halali na kupata malipo halali. Sura ifuatayo itajadili sababu za mabadiliko hayo.

# SURA YA TATU

## SABABU ZA MABADILIKO YA NAFASI NA MTAZAMO WA WAHUSIKA WANAUME

### 3.0 Utangulizi

Sura hii itabainisha sababu za mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika katika riwaya teule. Kazi yoyote ya fasihi haizuki katika ombwe tupu bali huwa ni mkururo wa tajriba za mwandishi pamoja na kadhia zilizomsibu. Hizi ni kama vile malezi, elimu, mazingira alimokulia, ndoa yake au zake, matukio ya kijamii na kihistoria, mikondo ya siasa na utawala, itikadi zake na hata falsafa yake (Senkoro,1998; Njogu na Chimerah,1999). Kulingana na Kazungu (1984), fasihi aghalabu humithilishwa na fikra na mtazamo wa mwandishi juu ya maisha na ulimwengu kwa jumla. Hivyo, lazima kuwe na jambo au tukio fulani lililomchoma mwandishi, alilohusiana nalo, aliloliona au alilosikia katika pita pita zake za maisha ya kila siku, lililomfuma hisia zake na kumuathiri kwa namna fulani, akaingiwa na ilhamu kwa sababu ya furaha au karaha, akachukua kalamu akalitungia riwaya, shairi au tamthilia.

Mtafiti anaunga mkono mawazo hayo yote kwani fasihi ni kioo cha jamii na huchota malighafi yake kwa jamii. Hivyo, matukio anuwai katika jamii hayana budi kuathiri mwandishi katika maudhui na hata namna anavyowachora wahusika wake.

### 3.1 Historia fupi ya mwandishi Said A. Mohamed

Ni wazi kuwa upo uhusiano wa karibu kati ya mwandishi na kazi zake za kisanaa. Hivyo maelezo kumhusu mwandishi yaani alipokulia, aliposomea, alipofanya kazi na kadhalika ni muhimu. Maelezo haya humsaidia msomaji kuelewa kazi za utunzi (Hirsch, 1967).

Said A. Mohamed alizaliwa Unguja mwaka wa 1947 na kusomea shule kadhaa za msingi na za upili kuko huko. Mnamo 1974, alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kusomea shahada ya B.A (Elimu). Kisha 1981, alihitimu chuo hicho na shahada ya uzamili (M.A) ya Isimu. Aidha, alifundisha katika Idara ya Kiswahili chuo hicho kwa muda mrefu. Kati ya miaka 1982-1985 alijiunga na Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani kwa shahada ya uzamifu. Baadaye alirudi kwao na kufanya kazi katika Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Unguja, kama mkurugenzi. Pia alikuwa mhadhiri aliyefundisha visiwani, vyuo vikuu vya Nairobi na Moi nchini Kenya na Chuo Kikuu cha Osaka, Japani. Fauka ya hayo, amekuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani alipokuwa akifundisha fasihi ya Kiafrika hadi mwaka wa 2013 alipostaafu na kurudi nyumbani, Zanzibar.

### 3.2 Sababu za mabadiliko ya nafasi na mtazamo

Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule yamesababishwa na mabadiliko ya mazingira ya utunzi, mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa.

#### 3.2.1 Mabadiliko ya kimazingira

Mazingira ya kiutunzi hubadilika jinsi muda unavyobadilika. Tunaafikiana na mawazo ya Kezilahabi (1976) aliyekuwa akizungumzia utanzu wa ushairi anasema kwamba watunzi hujishughulisha na utunzi kufuatana na mkondo wa wakati na mabadiliko yake. Yaani, mtunzi huongozwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake wakati wa utunzi au mabadiliko yanayoikumba jamii anayoishi. Hawateui wahusika wao kiholela bali huakisi hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati.

Naye Mutembei (2013), katika utafiti wake kuhusu hali na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili katika Tanzania, anarejelea tanzu mbalimbali za fasihi na kuonyesha kuwa; dhamira mpya

huibuka katika utunzi ili kusawiri mazingira kiwakati. Kwa mfano, kuhusu riwaya, anarejelea riwaya nne. Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (Chachage,2002) mwandishi anaandika kuhusu madhara ya kujiingiza katika soko huria bila kujiandaa na pia anaangazia kuwepo kwa watu wachache waliojaa ufisadi ambao unaiangamiza jamii ya Watanzania iliyoinukia katika maelewano ya kijamaa.

Aidha, kwenye riwaya ya *Pesa za Mawe* (Ulomi,2006) mwandishi anaangazia mjadala kuhusu biashara ya madini. Vile vile, biashara haramu ya madawa ya kulevya na madhara yake kwa jamii inamulikwa ndani ya riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie* (Mbogo,2002). Mwisho kwenye riwaya ya *Pambazuko Gizani* (Mboneko,2004), mwandishi anaonyesha mabadiliko miongoni mwa asasi za kidini ambapo watu wamefanya kanisa kuwa aina ya biashara.

Kutokana na utafiti huo, inabainika kuwa fasihi ya sasa ya Tanzania ni tofauti kabisa na ile ya hapo awali. Kwa ufupi, mabadiliko ya kimazingira huchochea waandishi kubadili dhamira na maudhui yao ili yaoane vyema na mazingira ya wakati mahususi kwa mfano maswala ya mauaji ya mazeruzeru ambayo hayakuwa miaka ya hapo awali.

Kulingana na Wamitila (2007), ndoa pia ina sura ya kisasa kando na ile ya kitamaduni kwa mfano wachumba hujipangia wenyewe. Japokuwa wanaume wanapigania masuala kadhaa ya asasi ya ndoa yasibadilishwe, Wamitila anasema kuwa asasi hii haina budi kubadilika kwa kuzingatia namna dunia ya sasa ilivyo kuliko kunga’ng’ania ukale.

Hivyo, mazingira ya utunzi wa riwaya ya *Utengano* yalikuwa ni tofauti na yale ya utunzi wa *Dunia Yao*. Yamkini mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule yalitokana na mambo yanayotendeka katika jamii halisi katika karne ya ishirini na moja. Mathalan, wanawake katika nchi za Afrika Mashariki sasa wamefaidi elimu ya kigeni ambayo

inawawezesha kufanya kazi za ajira na hivyo kuweza kumiliki mali sawa na wanaume. Fauka ya hayo, sasa wanaweza kukimu familia sawa na wanaume kwa mfano Bi. M na bintiye Yungi katika *Dunia Yao*. Hii ilisababisha nafasi ya mwanamme katika jamii kubadilika kwani awali, mwanamume pekee ndiye alikuwa mkimu wa familia.

Aidha, kutokana na historia fupi ya mwandishi, imebainika ya kwamba ametangamana na mazingira tofauti tofauti ya kijiografia na hivyo kushuhudia mabadiliko anuwai yanayozikumba jamii nyingi ulimwenguni. Usawiri wa kihalisia ni njia mwafaka ya kupenya na kumulika hali mahususi katika jamii. Aidha, ikumbukwe kuwa fasihi huchota malighafi yake kutoka kwa jamii halisi. Hivyo, huenda mazingira ya Kiafrika hususan Afrika Mashariki yalimfanya mwandishi kuwasawiri wahusika wanaume katika *Utengano* kwa namna tofauti na alivyowasawiri wahusika wanaume katika riwaya ya *Dunia Yao*.Hii ni baada ya kutangamana na ulimwengu mpana zaidi na kupata tajriba zaidi kuhusu masuala tofauti tofauti ya kimaisha kando na kushuhudia mabadiliko katika jamii za Afrika.

### 3.2.2 Mabadiliko ya kijamii

Kutokana na ukweli kuwa mwandishi ni mwanajamii, yeye huathiriwa sana na mambo yanayotendeka katika jamii hiyo. Baadhi ya mambo haya ni yale anayoshuhudia, kuambiwa na mengine kusoma vitabuni. Katika karne ya ishirini na moja, yameshuhudiwa mabadiliko makubwa sana katika bara la Afrika hususan Afrika ya mashariki. Nchi inayorejelewa katika *Dunia Yao* (haikutajwa kwa jina) inakaribia kusambaratika kutokana na matatizo ya ndani kwa ndani na pia nguvu zinazotoka nje. Yawezekana kuwa nchi hii ni mojawapo ya nchi za Afrika Mashariki hususan Unguja alimotoka mwandishi. Mojawapo ya nguvu za nje zinazorejelewa hapa ni utandawazi. Kwa kumulika na kuweka bayana mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa

wahusika wanaume, mwandishi alinuia kutufahamisha kuhusu utandawazi uliopo hasa katika karne hii na athari zake hasi na chanya. Mwandishi alitaka kuangazia masuala yanayozikabili jamii hasa za Waafrika. Hii ni kwa sababu alikwisha shuhudia jinsi ulimwengu umebadilika na kuwa ulimwengu unaoongozwa na kutawaliwa na mfumo wa utandawazi katika masuala yote kama vile uchumi na biashara, jamii au familia, siasa, dini na kadhalika. Hivyo mtu hawezi kujiepusha na utandawazi. Tomlinson (1999), alikiri kuwa utandawazi u katika kitovu cha utamaduni wa kisasa. Siku hizi mali, mtaji, watu, maarifa, picha, uhalifu, dawa za kulevya, ngono, mavazi na imani zote zinasambaa kwa urahisi na kuvuka mipaka. Hii inazua utamaduni mmoja ulimwenguni kote. Utamaduni huu unatupilia mbali tamaduni asilia za watu wa jamii na mataifa tofauti.

Zaidi ya hayo, kwa kumulika athari hasi (mbaya) za utandawazi, mwandishi alilenga kutahadharisha watu hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu ili wawe makini wasije wakaiga mambo yote au kukubali kuathirika kiholelaholela kwani yote yang'aayo si dhahabu. Mohamed (1999), ana maoni kuwa utandawazi si dhana mpya bali ni upeo wa dhana kongwe yenye sifa mpya ya kutumia maendeleo makubwa yaliyopatikana kiteknolojia, ili kunyonya kwa mapana na marefu; utajiri wa dunia na kuwaacha watu wa nchi maskini kuwa maskini zaidi. Pia, huwachafulia uchumi, utamaduni na maisha yao vibaya hadi kufikia nchi hizo kudharauliwa na kuonekana si lolote, si chochote katika fikra ya dunia ya leo.

Kwa upande mwingine, kwa kuangazia athari chanya (nzuri) za utandawazi, mwandishi alilenga kuhimiza watu wakubali maendeleo ya teknolojia na habari kwani yaweza kuwa ni chombo cha kutufahamisha njia mwafaka za kunawiri kiuchumi, kuboresha na kurahisisha mawasiliano na kadhalika. Katika riwaya ya *Dunia Yao* tunaelezwa:

> Tena kulikuwa na kuwasiliana na kusema na ulimwengu wote. Nako kulikuwa na faida na hasara zake. Hasa katika akili changa (Uk. 11).

Aidha mwandishi anatupa habari zaidi kuhusu utandawazi kwa kutueleza hivi:

> Linapiga kasi katika njia yake inayojiandika yenyewe – mara Globalization mara Americanization. Na lilipotimka lilitifua kila kitu dhaifu katika kasi na mikiki yake. Kila kitu kilipojaribu kufukuzana nalo, kilijikuta kinawachwa nyuma milioni ya kilomita. Likapita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likiripuka mandimi ya moto yaliyounguza na kukausha kila kitu: watu, wanyama, barabara. Majumba, miji na majiji, mashamba, mazao ya chakula, mazao ya mauzo…desturi, mila, tamaduni na hata uhai, heshima na mutakabali wa watu- hata roho zao. Lilipenya hata ndani ya nyumba na vibanda vya watu kusasambura na kupekua kila kitu, kukashifu na kufedhehi na kisha kuangamiza lilivyopenda. Liliingia humo na kutawala na kuamrisha na kulazimisha mambo katika nyumba yake mwenyewe mtu (Uk.205-6).

Ujio wa utandawazi ni mabadiliko makuu ya kijamii ambayo hayakushuhudiwa hapo awali. Utandawazi unaathiri maswala mengi ya kijamii kama vile desturi, mila, heshima, dini na tamaduni. Ni nguvu zisizoepukika katika karne hii. Utandawazi umepenya hata ndani ya nyumba na kuangamiza mpangilio na mamlaka katika familia. Hivyo unaathiri malezi na mahusiano nyumbani. Alsaedy (2015), ana maoni kuwa kutokana na utandawazi, kuna ukosefu wa maelewano kati ya wazazi na watoto wao. Ukosefu wa ushauri ufaao wa wazazi kwa watoto umechangia pakubwa kuwepo kwa tabia na mienendo mibaya. Vile vile, nafasi na mamlaka katika familia yamebadilika sana kutokana na wanawake kuanza kufanya kazi nje ya boma na kupata elimu, inayowafanya kutaka kutawala katika familia zao hivyo kuanza kuchukua nafasi ya wanaume. Fauka ya hayo, kupitia utandawazi, watoto na vijana wamepata maaarifa mengi mapya kuhusu utamaduni ajinabi na dhana mpya zinazopingana na mafunzo ya wazazi na desturi

za jamii zao. Wazazi nao wanajipata katika hali ya mtanziko kwani kuna mabadiliko mapya kwa upande wa tamaduni na amali za jamii zao asilia.

Naye Kgatia (2013) katika kuzungumzia utandawazi anasema kuwa, umevunja uti wa mgongo wa dini, utamaduni na elimu ya Kiafrika na zaidi ya hayo, umesambaratisha familia na mahusiano ya jamii nyingi. Kwa sasa, watu hupima thamani ya utu na ubinadamu wao kupitia vitu wanunuavyo na watumiavyo. Watu wamefanywa kuamini kuwa furaha yao na kutosheka maishani kunaweza kununuliwa kwa fedha. Aidha, wokovu unaweza kupatikana kupitia matendo mazuri wala si kwa neema ya Mungu.

Mohamed na King'ei (2008) wanasema kuwa utandawazi ni dude au nyangarika linalopita kila pahala kuhakikisha maslahi yake yanatimizwa kwa kutumia hila na nguvu. Utandawazi ni dhana ambayo imetapakaa katika kila nyanja ya maisha ya binadamu na huwezi kujiepusha nao kwani uko kila mahali mfano mito, maziwa, pwani na bahari, mfumo wa elimu, mikutanoni na kongamano zote. Zaidi ya hayo, wanaonyesha bayana kuwa utandawazi umeathiri desturi za jamii kwa mfano vijana wa siku hizi wanakwenda uchi kwa kuvaa mavazi yasiyositiri. Jambo hili ni kinyume na utamaduni wa Mwafrika. Pia wanatumia lugha isiyoeleweka na fikra zao pia hazieleweki. Nyimbo zao pia ni za kigeni kupitia vyombo vya kiteknolojia hivyo, fasihi ya kimagharibi imepokezwa Waafrika.

Raheem na Asim (2015) pia walifanya utafiti wa athari za utandawazi kwa utamaduni miongoni mwa wanafunzi kule Pakistani. Wanagundua kuwa tabia na hulka za wanafunzi zimeathiriwa na kubadilishwa sana na utandawazi. Aidha, utamaduni wa Magharibi unatawala sekta zote za maisha ya wanafunzi kuanzia vyakula, vinywaji, mavazi yao na lugha watumiazo. Hii imesababisha mmomonyoko wa tamaduni asilia na pia kupotea kwa maadili ya kidini. Haya ni

baadhi tu ya maswala ya kijamii yalioathiriwa na utandawazi. Inakuwa vigumu hata kwa wazazi kudhibiti watoto wao kitabia. Wanasalia tu kutazama wana wao katika dunia yao inayoendeshwa na utandawazi.

Hivyo ni wazi kuwa kutokana na mabadiliko mengi ya kijamii katika karne ya ishirini na moja, mabadiliko ya nafasi na mamlaka ya wahusika wanaume yameonekana.

### 3.2.3 Mabadiliko ya kiuchumi

Mabadiliko mengi ya kiuchumi yanadhihirika katika karne ya ishirini na moja. Kwanza kuna kupunguzwa kwa idadi ya wafanyikazi ambapo mwanamume anajikuta hana kazi tena. Utafiti uliofanywa na Stout (2012) unadhihirisha kuwa kuanzia mwisho wa miaka ya tisini kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanaume wanaokaa nyumbani baada ya kupoteza kazi zao. Takwimu zilionyesha kuwa wanawake wanne kati ya kumi ndio watafuta riziki katika familia zao huku takriban wanaume 143,000 wasio na kazi wakisalia nyumbani kulea watoto.

Dailey (2014) katika kutafiti sababu za kuwepo kwa kina baba wengi wanaokaa nyumbani katika mji wa New York anadhihirisha kuwa, idadi ya kina baba wanaokaa nyumbani na kulea watoto imeongezeka mara nne. Anasema kuwa kina mama wamepata kazi zenye mishahara mikubwa sana kuliko wanaume wao na hivyo hawawezi kusalia nyumbani. Aliwahoji baadhi ya kina baba waliomweleza kuwa wake zao walipandishwa vyeo kazini na kuongezewa mishahara na hivyo ikawalazimu wanaume kukaa nyumbani kulea watoto huku wake zao wakienda kazini. Aidha baadhi ya wanaume walisema kuwa hata kabla ya kuolewa, wasichana au wanawake huwa na kiwango cha elimu cha juu zaidi kushinda wanaume wao na hivyo wanapata kazi zenye mshahara bora zaidi.

Hapa nchini Kenya, katika utafiti wake Mburu (2016) anaonyesha kuwa, katika miaka ya awali, wanawake ndio walisalia nyumbani kulea watoto na kufanya kazi nyinginezo ndani ya boma. Hata hivyo, mambo yamebadilika kwa kasi kwani sasa kumezuka wanawake wenye mishahara mikubwa wanaozikimu familia zao huku wanaume wao wasio na kazi wakisalia nyumbani kulea watoto. Hata hivyo, kinyume hiki cha mambo kimezua athari nyingi ikiwemo wanawake kuwadharau waume wao na kutaka kuwadhibiti. Hali hii ikitokea wanaume huanza kuwa na hisia za kutotosheka, kutokuwa na uhakika kuhusu mustakabali wa ndoa zao na pia wanakuwa na ukinaifu. Wao hupoteza hadhi yao kama wanaume. Hali hii yaweza kuleta ugomvi au vita kati ya mume na mke kwani mwanamume hujawa na woga kuwa hatoi mchango wowote wa kifedha na kuhisi kuwa mwanamume mwingine yeyote mwenye kazi na mshahara bora atachukua nafasi yake katika ndoa yake.

Kulingana na Appleyard (2007), baadhi ya wanaume walilazimika kukaa nyumbani kutokana na matatizo ya kiuchumi yaliyoshuhudiwa huko Marekani kuanzia miaka ya elfu mbili ambapo viwanda vingi vilishuhudia hasara kubwa na hivyo kuwafuta au kupunguza idadi ya wafanyakazi wengi kati yao wakiwa wanaume.

Kutokana na tafiti hizi, inabainika kuwa mabadiliko ya kiuchumi katika taifa yanaweza kuibua mabadiliko katika nafasi ya mwanamume ya kuitafutia familia yake riziki. Hii ndiyo sababu tunawona Bi. M akichukua jukumu la kwenda kutafutia familia yake riziki huku mume wake akisalia nyumbani baada ya kufutwa kazi. Aidha, nyakati zimebadilika ambapo wanawake wengi wanapata mishahara ya juu zaidi ya ile ya waume zao kutokana na hoja kuwa wanawake sasa hupata elimu inayowawezesha kupata ajira. Hivyo, baadhi ya wanaume huamua kuacha kazi kabisa na kusalia nyumbani na watoto. Mwisho, wanaume ambao tangu kitambo wamekuwa

watafuta riziki wanaweza kupata magonjwa na kushindwa kuendelea na kazi. Inambidi mke achukue jukumu hilo.

### 3.2.4 Mabadiliko ya kisiasa

Salisu (2004) anasema kuwa, baada ya nchi nyingi barani Afrika kujinyakulia uhuru, bado watawala wazungu waliendelea kudhibiti uchumi wa nchi hizo. Jinsi ulimwengu ulivyoendelea kupitia mabadiliko mbalimbali, ukoloni mamboleo uliendelea kukithiri. Kuliibuka mbinu mpya ya unyanyasaji kupitia utandawazi. Hata sasa, kuna uthibiti wa watu na raslimali katika nchi nyingi za Afrika katika misingi ya utandawazi kupitia mashirika kama vile Shirika La Fedha La Dunia (IMF) na Shirika la Biashara la Dunia (W.T.O).

Katika utafiti wake akilenga tamthilia teule, Mwirabua (2014) anagundua kuwa mfumo wa utandawazi unatumiwa kubebea matakwa ya wakoloni na pia vibovu vyao kwa mataifa maskini. Ijapokuwa bara la Afrika limerembeshwa kwa rasilmali mbalimbali kama vile madini, watu wenye ujuzi, mito na maziwa ambayo hayajatumika ipasavyo, hakuna viongozi wenye maono ambao wangetumia vitu hivyo kuendeleza mataifa ya Afrika.Utandawazi umetumika kubomoa bara la Afrika si kisiasa tu bali pia kijamii. Hata hivyo, Mwafrika anapaswa kujilaumu mwenyewe kwa sababu ya maovu na balaa inayomkuta kwani uongozi mbaya unakubali chochote kutoka kwa wazungu. Waafrika wanafaa waamke na kupigania haki zao na umoja wao wa ndani na wa nje.

Baadhi ya mabadiliko yaliyojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao*, yanasababishwa na hali nzuri au mbaya zinazosababishwa na mifumo ya kisiasa. Baadhi ya wananchi walitemwa kazini kwa sababu ya kutounga mkono viongozi fulani wabaya. Walipokosa kushirikiana nao, walitupwa nje na hivyo kupoteza kazi zao. Hii ni baada ya wafanyakazi hao kugundua kuwa viongozi wao ni

walafi na wanaendeleza ukoloni mamboleo ilhali ni miaka mingi baada ya nchi kupata uhuru. Matunda ya uhuru yanaendelea kufurahiwa na wachache walafi ilhali umma unaendelea kutaabika. Hii ni kuonyesha ukosefu wa uthabiti wa nchi za Afrika hasa Afrika Mashariki. Wananchi waadilifu wanatemwa kando eti kwa sababu ya kugoma kuhusiana na viongozi wabaya. Kunakuwa na migogoro ya kisiasa kutokana na dhuluma za walio mamlakani au waliohodhi nyenzo za kuzalisha mali.

Ndi- anapokataa kuunga mkono viongozi wanaoendeleza dhuluma na ubinafsi wa mkoloni mkongwe, wanaanza kumtenga na kumkejeli. Tunaelezwa:

> Mwaka mzima sasa tokea nigome kula au kunywa chochote katika sherehe na karamu zilizoandaliwa ofisini. Mwanzo nilikuwa mwoga kusema kwa nini. Nilipoulizwa nilijitia nimo katika saumu. Funga ya Ramadhani ya milele. Baadaye ishara za kutengwa na wakubwa wote wa ofisi hii niliziona kwa mbali. Nilipohudhuria vikao vyao vya mlo wa aina hii, matamko ya kejeli yalitolewa wazi. Nikiambiwa mimi kwa vijembe. Eti wale wanaojitia hisia wasizokuwa nazo wafe tu! Ilisemwa wazi asiyetaka kushiriki katika mlo ule asihudhurie kamwe. Awache kazi! (Uk. 81)

Baadaye anaposimama kidete na kuwakashifu kwa dhuluma, tamaa na ubinafsi wao, wanamwitia polisi. Anakamatwa na pia kufutwa kazi na hili linamfanya aathirike sana Anakosa mamlaka ya kuithibiti familia yake kwani hata kuitimizia mahitaji ya kimsingi hawezi. Pia hali hiyo inatudhihirishia mtazamo wake kuhusu kazi na malipo halali.

### 3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha sababu za mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule. Usawiri wa wahusika na hata maudhui katika fasihi hubadilika sambamba na mabadiliko katika mazingira ya mtunzi. Hii ni kwa sababu yanayotendeka katika jamii humchochea mwandishi kuyasawiri katika fasihi. Pia, mabadiliko ya kijamii katika karne

ya ishirini na moja yameibua mabadiliko mengi ya nafasi ya mume katika ndoa na mzazi wa kiume katika familia. Kwa mfano, wanawake kuelimika, athari za ujio wa utandawazi na kadhalika. Mwisho, mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa yamechangia kubadilisha nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume. Mathalan, ugumu wa maisha ya sasa kiuchumi, ajira ya wanawake na pia kukita mizizi kwa ukoloni mamboleo uliojificha kwenye misaada kumechangia pakubwa kuzua mabadiliko hayo.

# SURA YA NNE

## ATHARI ZA MABADILIKO YA NAFASI NA MTAZAMO WA WAHUSIKA WANAUME KATIKA UENDELEZAJI WA RIWAYA KIMAUDHUI

### 4.0 Utangulizi

Mabadiliko katika jamii yoyote ile yawe ni ya kiuchumi, kisiasa, kijamii au hata kimazingira, huiathiri pakubwa kazi yoyote ya fasihi. Athari hii huonekana katika uteuzi wa mada, usawiri wa wahusika na pia maudhui. Maudhui ni kipengele muhimu sana katika kazi ya fasihi kwani maudhui ndiyo yanatufahamisha mafunzo na mawazo ya mwandishi. Hayazuki tu bali huhusishwa na hali halisi za kisiasa, kijamii na kiuchumi zilizomzaa, zilizomlea na kumkuza msanii. Hivyo, matukio makuu ya mwongo fulani yaweza kutambulika kutokana na fasihi ya mwongo huo haswa tunapochunguza kipengele cha maudhui kwa vile ni 'kioo cha jamii' na hubadilika kiwakati kadri jamii inavyozidi kukumbwa na mabadiliko (Creig,1975). Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule yamezua maudhui mengi ambayo yamesaidia kuendeleza riwaya kimaudhui.

### 4.1 Mmomonyoko wa maadili

Kutokana na mabadiliko ya kijamii hasa ujio wa utandawazi, tamaduni na maadili ya kigeni yameingizwa katika bara la Afrika. Maadili mema yaliyokuwa yakihimizwa katika jamii za Kiafrika tangu zama za kina babu zetu yametokomea na kutupwa katika kaburi la sahau. Kgatia (2013) anasema kuwa, kupitia vyombo vya habari na burudani kwa mfano televisheni, radio, mtandao, magazeti, filamu na video, utamaduni wa magharibi umesambazwa ulimwengu kote. Matokeo yake ni kuwa vijana wameshawishiwa kuuenzi na kuutekeleza utamaduni huo bila kuweka mipaka.

Kulingana na Oni (2003), utamaduni wa magharibi ambao umeenezwa kote Afrika kupitia utandawazi umeathiri sana maadili na amali za Kiafrika. Elimu asili ya maadili ya Kiafrika iliyokuwa ikihimiza heshima kwa watu wazima, utiifu, wema, upendo na umoja, imewekwa kando huku elimu ya kimagharibi ikihimizwa. Vijana wa Afrika wamefanywa kuamini kuwa utamaduni wowote wa Kiafrika na unaohusiana na watu weusi haufai, hauna maana na umepitwa na wakati ilhali utamaduni wa Magharibi wa watu weupe ndio bora na ufaao kutekelezwa. Basi utamaduni huo wa wazungu uliojificha katika elimu tunayopata kwa sasa na pia vyombo vya habari na mawasiliano, unapitishwa pole pole kwa watoto na vijana na kudaiwa kuwa huo ndio usasa. Vijana Waafrika wamefanywa kujichukia na hivyo kuiga mitindo ya mavazi, tabia, nyimbo, mitindo ya nywele na hata lugha ya Wazungu huku wakidharau lugha yao asili. Hii inaaminika kuwa ndio ustaarabu.

### 4.1.1 Watoto kuwakosea wazazi heshima

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, Yungi aliwakosea wazazi wake (Ndi- na Bi. M) heshima kwa kuwazungumzia jinsi alivyotaka. Anamweleza babake:

> Uukubali ukweli. Wakati umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Pia huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume (Uk. 25).

Mamake anapojaribu kumwonya Yungi anyamaze, Yungi anamweleza:

> Nyamaza na wewe, kama miaka hii yote umeshindwa kumzuia bwana huyu kuwa mwamba katika nyumba hii… (Uk. 25)

Badala ya watoto kunyenyekea mbele ya wazazi wao na kuwazungumzia kwa heshima, katika karne ya ishirini na moja watoto wamebadilika. Kwa sababu ya athari za utandawazi, watoto wa Afrika wameiga uhuru wa watoto wa Kizungu wa kuwajibu wazazi watakavyo. Aidha

inadhihirika kuwa nafasi ya mwanamume ya kuiongoza na kuikimu familia yake inapobadilika mume hawezi kuendelea kuheshimiwa na kuhudumiwa kama mume au baba.

Baadaye, tunaona mawazo ya Ndi- kuhusu jinsi utandawazi umeathiri maadili ya watoto:

> Hakuna adabu, heshima au kujaliana. Hakuna ubaba wala ubinti. Haya ni mambo ya kale. Na mambo ya kale ni mambo ya kale. Hayana maana. Yameshapitwa na wakati. Yungi anaweza sasa kunikabili na kuniambia analotaka bila ya kisisi wala kiwewe. Uwazi ulioje! Uwazi wa usasa. Uwazi wa usasa baadaye kusema kweli. Upepo unavuma. Unaangusha mibuyu na kuporomosha majengo aushi. Unapigana kubadilisha kila kitu (Uk. 107).

Nguvu za upepo wa utandawazi zinaonekana wazi katika karne ya ishirini na moja. Utandawazi umekuja kuchafua na kubomoa tamaduni zetu zilizokuwa kama majengo aushi. Heshima iliyokuwa kati ya watoto na wazazi wao haipo tena. Watoto sasa wanaweza kuwazungumzia wazazi wao kwa ujeuri wote bila kuogopa hata laana ya wazazi. Jambo hili halikushuhudiwa kamwe katika miaka ya hapo awali. Kwa upande mwingine, wazazi wanahuzunikia watoto wao kwa sababu watoto hawafahamu hatari iliyomo ndani ya usasa na uhuru wautakao wa kutenda na kusema watakavyo.

### 4.1.2. Uasherati

Ambrose na Palm (2015) wanasema kuwa utamaduni wa magharibi umebadilisha mawazo na fikra za watu kuhusu uchumba. Katika karne ya ishirini na moja, vijana hawajishughulishi kutafuta mtu wa kuchumbia au kuwachumbia kwa nia ya kuoa au kuolewa. Wengi wao hutafuta mtu wa kujiburudisha naye tu kisha wanaachana. Pia waligundua kuwa, miaka michache iliyopita, watu walikuwa wakichumbiana ili kuwa na mahusiano ya kudumu. Hata hivyo, katika karne ya sasa mahusiano mengi ni ya kingono kabla ya kuwazia chochote cha uzito kama vile

ndoa. Vituo vya mtandao humpa mtu idadi kubwa ya watu anaoweza kuchumbia na inakuwa vigumu kuchagua. Badala yake mtu huamua kufanya urafiki wa ngono za kiholela na mtu mmoja baada ya mwingine.

Hii inazua uasherati mwingi kati ya vijana hawa na madhara yake ni mengi kwa mfano magonjwa ya zinaa. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, inabainika kuwa mwanamume anapokoma kuwaadhibu watoto na kuidhibiti familia, watoto wa kike wanajiingiza katika uasherati wa hali ya juu. Baadhi ya watoto hao wanadai kuwa wanajiingiza katika usherati ili watafute riziki kwani baba zao wameshindwa. Yungi, bintiye Ndi- anajiingiza katika uasherati. Anavalia mavazi mafupi yaliyombana na hata kujihusisha kimapenzi na wazungu. Anawaleta wanaume pale nyumbani kwa babake na kushiriki raha ambazo Ndi- anaziita za kishetani. Madhara yake ni kuwa Yungi anapata ugonjwa wa zinaa. Ndi- anajua haya kupitia kwa bintiye mdogo Kilua anapomweleza:

> Yungi anaumwa na maradhi mabaya. Niliingia chumbani mwake na kukiona cheti chake cha hospitali. Kimeandikwa maradhi mabaya ya uasherati (Uk. 92).

Hivyo kwa kuwa wanaume wamekoma kuadhibu, kushauri na kuelekeza watoto wao, mabadiliko hayo ya kimaadili kati ya mabinti yanadhihirika. Tunaona kuwa wanaume wameuacha utandawazi uharibu kila kitu. Hatuwaoni wakijaribu kwa upande wao ili kudhibiti mambo. Licha ya kuwa utandawazi una nguvu katika karne hii, wazazi wa kiume wangejaribu kutekeleza jukumu lao kwa kutokata tamaa. Pengine mambo hayangeharibika kwa kiasi kikubwa namna tuonavyo sasa.

### 4.1.3 Matumizi ya dawa za kulevya

Kutokana na utandawazi, wazazi wa kiume wameshindwa kuzidhibiti familia zao. Vijana wengi wa kike na kiume wameshinikizwa na utandawazi kujiingiza katika ulevi wa dawa mbalimbali kupitia vyombo vya habari na mawasiliano. Zaidi ya hayo, wanashiriki anasa za kupindukia kwa mfano kushiriki densi za kisasa kwenye vilabu. Hivyo watu wazima wanalazimika kuamini kuwa, vijana ni tofauti kabisa na kizazi cha wazee na wanahofia kuwa utamaduni mgeni umevamia maadili ya jamii za Kiafrika (Mishra, 2004).

Kama bendera ifuatavyo upepo, vijana wanaonekana kufuata mkondo huu mbaya unaowaathiri vibaya. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, vijana wengi wanaonekana kutumbukia katika dawa za kulevya kwa mfano pombe, sigara na hata kokeini. Kwa mfano, Yungi alizoea kurudi nyumbani usiku wa manane akipepesuka kwa ulevi wa pombe. Pia, katika kisa kingine Kilua anapoingia chumbani mwa Yungi na kusoma cheti cha hospitali kilichoonyesha kuwa Yungi alikuwa na maradhi ya zinaa; Kilua alimfahamisha babake Ndi- kuwa:

> Aliingia ndani ghafla da Yungi. Alinipiga kibao na kunichoma moto kwa sigara aliyokuwa akivuta (Uk. 93).

Fauka ya hayo, Jitu (mwanawe Ndi-) anashiriki ulevi wa kokeini unaomfanya kuwa na mtindo wa kuuza vitu vya nyumba zikiwemo nguo, redio na tepurekoda ya Yungi. Yamkini Jitu anambaka dadake mdogo Kilua kutokana na ulevi huu wa dawa. Yungi anapompeleka Jitu polisi kwa sababu ya kumwibia, anakaa kule jela kwa muda wa saa moja tu kwa sababu walevi wenzake wanaununua uhuru wake kwa kuwahonga polisi. Tunaelezwa:

> Yungi alilalamika kwamba Jitu ana mtindo wa kuuza vitu vya nyumba kununua unga. Alianza kuuza khanga ma kanzu za Yungi, lakini jana aliuza redio na teprikoda yake. Yungi alipolalamika Jitu alimpiga kigongo cha kichwa Yungi. Walipelekana polisi, lakini

> alikaa ndani saa moja tu jitu. Watumiaunga wenzake waliununua uhuru wake polisi (Uk. 101).

Zaidi ya hayo, vijana wawili wa bwana Ndera waliishia jela ya wendawazimu kutokana na matumizi ya kokeini. Tunaelezwa:

> Isitoshe, vijana wake wawili wameishia jela ya wendawazimu kwa unga. Mmoja kafungwa jela kwa wizi (Uk. 129).

Uraibu huo wa dawa una mizizi katika nchi nyingi za ng'ambo. Tunang'amua hayo kupitia barua pepe ya Mtima kwa babake Ndi- alipomweleza jinsi baadhi ya vijana wameambulia kula madawa ya kulevya na kujitia katika mizozo na hatari.

Mifano hiyo yote ni dhihirisho tosha kuwa matumizi ya dawa za kulevya kati ya vijana wa kike na kiume yamewavuruga akili na kuwafanya wawakosee wazazi wao heshima. Aidha, wanatokwa na utu hivi kwamba wako tayari kutekeleza uovu wa aina yoyote ile kama vile kuwaumiza watu wengine wakiwemo ndugu zao. Wengine wanavurugika akili kabisa na kuishia hospitali za wendawazimu. Vijana hawa wanakuwa hatari kwa wazazi wao na jamii nzima. Baadhi yao wanadhubutu hata kuwaibia wazazi wao au kuuza vifaa vya nyumbani ikiwemo samani. Kinaya ni kuwa, wazazi wa kiume wamekaa kando kabisa na hawaonekani wakidhibiti watoto wao na matokeo yanakuwa ni kama hayo ya ulevi wa dawa.

### 4.2. Ukosefu wa kazi na athari zake

Kulingana na Holter na wengine (2009), kwa kuwa utu uzima unasawazishwa na kazi; basi kukosa kazi, kufutwa kazi au hata kupata mshahara mdogo sana kunasababisha mtu kutotambuliwa na jamii kama mtu mzima. Kwa wanaume wengi pia, kukosa kazi kunasababisha aibu na hata kuathirika kiakili. Vijana nao wakikosa kazi, hujiunga na vikundi vya uhalifu na

kutekeleza uvamizi na ubakaji. Vile vile, baadhi ya vijana wakikosa kazi huamua kwenda nchi za ng'ambo kutafuta kazi au kuendeleza masomo ya juu.

Utafiti wa shirika la kimataifa linalohusiana na kazi (I.L.O, 2016), wa kipindi cha miaka 1996-2016 unabaini kuwa thuluthi mbili ya vijana katika baadhi ya mataifa yanayokua ama hawana kazi au wanafanya kazi zenye mapato duni. Kati ya nchi sita juu ya kumi zilizotafitiwa, zaidi ya asilimia sitini ya vijana hawana kazi au wanafanya kazi zisizodumu za mishahara duni aghalabu katika sekta ya jua kali. Hivyo, ili kutatua shida hii shirika hilo lilisema kuwa kiwango cha elimu kinastahili kuboreshwa. Aidha, miundo misingi inafaa kuboreshwa na pia kuwe na utawala bora katika mataifa hayo. Hata hivyo, shirika hilo pia lilisema kuwa japokuwa viwango vya elimu vimeongezeka katika baadhi ya mataifa, bado haitoshi kwani ni watu wachache tu wamefuzu elimu ya shule za upili.

Fauka ya hayo, kutokana na ongezeko la idadi ya watu katika bara la Afrika; vijana zaidi ya milioni 600 wanang'ang'ania nafasi milioni 200 za kazi. Hivyo, inakuwa vigumu kwa watu kupata riziki sembuse kazi za kudumu. Utafiti wa shirika la ulimwenguni linalohusika na tafiti za kiuchumi na fedha unawiana na huo kwani unaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la ukosefu wa kazi katika mataifa yanayokua kwani kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu. Pendekezo lingine lililotolewa na shirika hilo la kazi ili kuleta suluhu ni kupanua na kuimarisha sekta za utalii, usafiri, afya na elimu kwani hii itaunda nafasi za kazi na kukomesha umaskini.

Katika riwaya teule, maudhui ya ukosefu wa kazi yanaonekana katika *Dunia Yao*. Mhusika Ndi- anapoteza kazi yake katika ofisi ya serikali. Kazi hiyo ndiyo ilikuwa ikimwezesha kuikimu familia yake. Baada ya Ndi- kufutwa kazi, anashindwa kuendelea kuwaelimisha watoto wake vyema hivyo wale ambao wangeishia kupata kazi baadaye, hawakuwa na kazi. Pia alishindwa

kuilisha familia yake hivyo mke wake analazimika kuanzisha biashara ndogo ili angalau watoto wake wapate chakula. Fauka ya hayo, wale walioelimika kwa kiasi fulani bado hawajapata kazi kutokana na kutokamilisha masomo. Hata Mtima, bintiye Ndi- aliyekwenda Uingereza, hakufanikiwa kupata kazi huko. Kupitia barua pepe kwa babake, alimweleza kuwa kwa miezi minane hakuwa na kazi ila ya kufagia na kufuta mavumbi dukani. Kazi zilizokuwepo zilikuwa chache na kugombaniwa na kila mtu, wakiwemo Warusi na jamaa wa Ulaya ya Mashariki. Watu wengine walishinda mabarazani wakizembea. Mtima aliishia kupatwa na maradhi ya kiakili. Naye Yungi alimweleza babake Ndi-:

> Hizi 'A' nilizonazo katika shahada ya kidato cha sita zinasaidia nini? Mwaka wa saba huu sijapata kazi wala nafasi ya kuingia chuo kikuu kwa ukosefu wa malipo na ukweli kwamba mimi ni binti yako (Uk. 105).

Iwapo wanaume waliofutwa kazi kama Ndi- wangejipiga vifua na kuamua kutafuta kazi nyingine, wangeendelea kuimudu karo ya watoto wao hivyo basi watoto hao wangekamilisha masomo. Kwa namna hiyo, ingekuwa ni rahisi kwa watoto wao kupata kazi kwani kuna mashindano makubwa katika nyanja za kazi kulingana na utafiti wa shirika la ulimwenguni linalohusika na masuala ya fedha na uchumi (W.E.F , 2016).

Kulingana na utafiti uliofanywa na shirika hilo, nafasi za kazi zimeongezeka katika mataifa yanayokua. Kwa upande mwingine, viwango vya elimu bado viko chini na pia idadi ya watu ni kubwa. Kwa mfano, katika sekta ya kilimo, mashine zimeanza kutumiwa sana ila ni watu wachache mno wenye ujuzi wa kuziendesha hivyo wanabaki bila kazi.

### 4.3 Kukata tamaa maishani

Winerman (2005) alifanya utafiti na kugundua kuwa, wanaume wanapokuwa na matatizo, huwa ni vigumu kwao kuonyesha hisia kwani huwa hawataki kuonekana wanyonge. Dalili za kuathirika kwao kiakili huwa ngumu kuzitambua hata na wale wapendwa wao kwani wanaume huwa hawakiri shida zao wala kudhihirisha hisia. Baadhi ya dalili hizo kwa wanaume ni kukosa usingizi, kufa moyo na kukata tamaa maishani. Wanakuwa na mawazo mengi sana kujihusu na kuhusu ulimwengu. Inakuwa vigumu kwao kufanya kazi na wakiifanya, hawaitekelezi ipasavyo.

Wengi wao huanza kujitenga na watu. Wao huona vigumu kudumisha mahusiano na watu wengine au hata kuwasiliana nao. Aidha, huwa hawana hamu ya mapenzi kwa wake zao. Hivyo wanakosa ujasiri na kuepuka kuzungumza nao (Eaton, 2011). Wanaume wanaoathirika zaidi ni wale ambao wanatambua kuwa nafasi zao kazini, katika mahusiano na katika jamii kwa jumla zimebadilika kwani wameishi kwa muda mrefu katika mazingira yanayotawaliwa na mfumo wa kuumeni.

Wahusika wa kiume wameibua maudhui ya kukata tamaa kutokana na mabadiliko yao. Kwa kuona maovu yanayoendelea katika jamii ya karne ya ishirini na moja, wanaume wameathirika kisaikolojia na kuwa kama wendawazimu. Ule ujasiri na ukakamavu uliohusishwa na wanaume katika jamii nyingi za kiafrika, hauonekani tena. Wamekuwa ni viumbe wa kujitenga na wengine na hata kujifungia vyumbani. Badala ya kujitokeza na kujaribu kuwaokoa watoto wao kutokana na uovu wa dunia ya sasa ulioletwa na utandawazi, wao wamekufa moyo kabisa. Wamekosa matumaini maishani.

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, badala ya wanaume kutafuta kazi nyingine, wanabaki kuomboleza ndani kwa ndani kama vile Ndi-, na wengine kulia wazi wazi kama vile Sakarati. Bwana Silima anamkejeli Sakarati kwa kulia:

> Mtazame analia. Baradhuli nini wewe? Nyamaza. Jikaze kidume. Ndio ulimwengu. Unamlilia nani asiye na mzigo wake? Pengine mkubwa zaidi kuliko wako! (Uk.52)

Hatuwaoni hata wakijaribu kuanzisha biashara yoyote. Ni kana kwamba wanaona hakuna lolote wangeweza kubadilisha na kufanya maisha yao bora. Vile vile, wanaamini kuwa hakuna mtu anaweza kukomesha athari za utandawazi.

**4.4 Kukita mizizi kwa ukoloni mamboleo**

Tafiti zimebaini kuwa katika karne ya ishirini na moja, ukoloni mamboleo unaendelezwa kupitia njia mpya na tofauti. Kwa mfano, Kothari (2006) anabaini kuwa ukoloni mamboleo unaendelezwa kupitia misaada ya kifedha kutoka nchi za kigeni. Hii ni kwa sababu misaada hii huwekewa masharti mengi. Kupitia kwa taasisi za kifedha kama Benki Kuu ya Dunia na Shirika la Kimataifa la Fedha, nchi za magharibi hutoa misaada ya kifedha huku wakishinikiza nchi zisaidiwazo kuhimiza uongozi bora unaounda taasisi za kiutawala zinazofanana na za nchi za magharibi. Jambo hili hufanikishwa kupitia utandawazi katika vyombo vya habari na mawasiliano. Nchi za kigeni hunuia kupata raslimali hivyo kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi na kisiasa (Harvey, 2003).

Kwa kuwa bara la Afrika linaogelea katika umaskini, njaa, magonjwa, ujinga na vita vingi, nchi za magharibi hudai kuleta misaada ya kifedha ila nia ni kujinufaisha. Kupitia taasisi kama vile Benki Kuu ya dunia, sera hutungwa na kulazimishiwa nchi maskini. Hivyo, nchi hizi huendelea

kutegemea uchumi wa magharibi. Aidha, wao huhimiza ubepari na kukashifu ujamaa. Hali hii hukuza watu wenye ulafi na ubinafsi mwingi na pia kunazuka matabaka ya maskini na matajiri.

Nnamdi (2016) akichunguza jinsi nadharia ya ukoloni mamboleo ya Kwame Nkrumah inavyobainika katika karne ya ishirini na moja, anaonyesha jinsi nchi za magharibi hueneza ukoloni mamboleo. Wao husambaza dhana za kigeni kati ya wananchi wa mataifa yanayokua. Dhana hizi ni za kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kudunisha dhana za kiasili. Hivyo, Waafrika wanaishi kuwategemea na kukubali dhana hizo mpya. Kulingana na Nkrumah, nia ya jumla ya ukoloni mamboleo ni kudhibiti na kutawala wengine kiuchumi huku watu wachache wakifaidi. Ni kuendeleza sera za kikoloni huku wakiwakidai kuleta uhuru na misaada.

Zaidi ya hayo, nchi za magharibi hujihusisha na miradi ya kuboresha hali na viwango vya Waafrika. Matokeo huwa ni rasilmali za Afrika kunufaisha uchumi wa nchi hizo za Amerika, Uropa na pia Ujapani. Mataifa hayo hung’ang’ania madini na rasilmali nyinginezo Afrika huku wakidai kusaidia Waafrika. Ukoloni mamboleo wa kitamaduni nao huendelezwa kwa kuhimiza ufundishaji na uzungumzaji wa lugha za kigeni. Basi, lugha asilia za watu hudunishwa na hatimaye kupotea huku lugha za wachache zikihimizwa ulimwenguni. Vile vile, misaada ya dawa, warsha za kidini na michezo mbalimbali hutumiwa kwa nia iyo hiyo.

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, ukoloni mamboleo umebainika wazi. Kwanza, viongozi wa Afrika waliochukua hatamu baada ya mkoloni kuondoka walionekana kuendeleza dhuluma kwa Waafrika wenzao. Aidha, waliongozwa na ubinafsi na tamaa ya hali ya juu. Lao lilikuwa kujinufaisha kwa fedha na mali huku wakitelekeza umma uliowachagua. Pale kazini Ndi-anasimama kidete kukashifu tamaa na ubinafsi wao wakati wa sherehe. Anasema:

> Hakuna udugu kuna uhasama wa mt una mtu. Hakuna sisi katika dunia hii! Kuna mimi! Kila kitu ni mimi, na mimi, na mimi… hakuna usafi wa sote ila uchafu wa mtu binafsi. Mnakula nini? Hamwoni? Hamjui kwamba mnakula mizoga? Hamjagundua kwamba mnafakamia mafunza na matapishi? Ishara ziwe zipi zaidi kuliko hizi? (Uk. 84)

La mno ni kuwa wanakubali uhusiano usio na manufaa kwa wananchi kupitia mfumo wa utandawazi. Mkoloni amejificha katika utandawazi na anasikika katika nyanja zote za maisha ya Waafrika. Kupitia juhudi za Yungi tunang'amua kuwa wazungu wamekita kambi katika mataifa ya Afrika huku wakiendeleza maslahi yao wakisaidiwa na viongozi weusi. Ndio maana watu wanaandamana kupinga mambo kama haya. Tunaelezwa:

> Si unajua kwamba wanataka kuvunja nyumba za eneo letu hili lote kwa kujenga hoteli ya Wataliana? (Uk. 210)

Zaidi ya hayo, Ndi- anatuelezea kuhusu sherehe na karamu zilizoandaliwa ofisini alipokuwa akifanya kazi. Yeye alikuwa ameamua kususia sherehe hizo na hivyo basi akaanza kutengwa na wakubwa wake na baadaye kufutwa kazi. Alikuwa amegundua kuwa viongozi walikuwa wanajihusisha katika mambo ya kujitajirisha, kujifaidi, kula jasho la mwananchi. Anapofutwa kazi, bintiye Yungi anamweleza:

> Mambo umeyaharibu baba. Sisi kwa kiasi chetu tulikuwa tumeketi pahala pema. Hatukuwa chini kamwe. Zamani kauli yako ilisikilizwa. Ulipokuwa afisa mtii wa serikali. Ulipokuwa ukishirikiana na kusikilizana na wakubwa. Kama ungaliendelea usingalikuwa hivyo ulivyo hivi sasa. Na sisi tusingalikuwa hivi tulivyo. Kama ungefuata mkondo kimyakimya bila kudhidi kitu chochote. Lakini ulianza kuhujumu watu wakubwa. Matokeo yake umejiharibia wewe Maisha yako na umetuharibia sisi yetu (Uk. 106).

Badala ya matunda ya uhuru wa nchi kufaidi umma, yaliwafaidi viongozi wachache na watu wao. Kando na tamaa ya viongozi, ubaguzi na ukabila wa hali ya juu unashuhudiwa kazini. Hizi

ndizo baadhi ya nguvu za ndani kwa ndani zinazotishia kusambaratika kwa nchi nyingi barani Afrika. Tunaelezwa:

> Baada ya mageuzi, kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara. Muhimu zaidi wewe ulikuwa nani mtoto au mjukuu wa bwana gani na kama unaitikia 'ndiyo' kila wakati (Uk. 16).

Mapendeleo kwa misingi ya kikabila na kadhalika yanakuwa na athari kubwa sana katika karne ya ishirini na moja. Walioelimika vyuoni hawapati kazi kutokana na ukabila na ubaguzi wa wanaoshughulikia nyadhifa za kazi. Wao wanaendeleza ubinafsi wa mkoloni mkongwe wa kuwafaidi wale tu anaohusiana nao kidamu au kikoo. Utu na haki hazifuatwi katika karne hii. Ukoloni mamboleo ulioanza miaka ya sabini na themanini umeongezeka sana na kuchukua sura mpya katika karne ya ishirini na moja.

### 4.5 Malezi

Alsaedy (2015) anaonyesha kuwa, wazazi wa sasa hutangamana kwa nadra sana na watoto wao. Hawazungumzii masuala muhimu kama urafiki na mabadiliko kutoka utotoni hadi utu uzima. Ukosefu wa ushauri ufaao unachangia pakubwa kuwepo kwa mienendo mibovu. Hii ni kwa sababu watoto na vijana hujipata katika hali ya mtanziko kutokana na mabadiliko mapya. Hawajui iwapo wafuate amali asilia za jamii zao au wafuate mapya waonayo kupitia utandawazi. Zaidi ya hayo, baadhi ya kina baba wanakiri kutowaelewa watoto wao kimawazo katika karne hii ya mtandao na basi wanashindwa kuwashauri (Siraji, 2007). Kupitia mitandao ya kijamii watoto hujifunza maswala mengi hasa yanayohusu uhuru wa mtu binafsi. Dhana hizi huathiri tabia na fikra zao. Aidha, baadhi ya dhana hizi huchukua nafasi za mafunzo waliyopata kutoka kwa baadhi ya wazazi wao (Chau, 2009). Hivyo, kutokana na mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume, maudhui ya malezi yanajitokeza.

Umuhimu wa wazazi kuwa vielelezo vyema kwa watoto wao unaangaziwa. Ndi- anapofutwa kazi, anashindwa kukabiliana vyema na changamoto hii. Hivyo anashindwa kuwajibikia majukumu yake kama kiongozi wa familia, mtafuta riziki na hata mdhibiti familia. Anapoteza mwelekeo anapokata tamaa maishani. Kwa namna hiyo anakuwa kielelezo kibaya kwa watoto wake na tunawaona wao pia wakikosa mwelekeo maishani. Wanapotoka kimaadili kwa kukosa mzazi wa kuwarekebisha, kuwashauri na hata kuwaadhibu wakosapo. Fauka ya hayo, Ndi- anajitenga na familia yake na hivyo ushawishi wake kama baba na mdhibiti wa familia unaisha kabisa. Wanafuata njia ile ile aliyofuata Ndi-. Kwa mfano kule Uingereza, Mtima alipokosa kazi mwishowe anakuwa mwendawazimu. Katika mojawapo ya barua pepe alizomtumia babake Ndi-, Mtima anamweleza:

> Ingekuwa jambo bora kwangu kama wewe na mama mngepinga kuondoka kwa-ngu. Mngenizuia. Ningekuwa na nafsi yangu tu kuilaumu (Uk. 116).

Suala la malezi linaangaziwa hapa ambapo watoto wanaonekana kuwalaumu wazazi wao kwa kutowashauri vyema kuhusiana na maamuzi mabaya. Wazazi kutowakanya watoto wao dhidi ya kuenda ulaya kutafuta kazi pasi na matayarisho mema mfano ya kielimu, kunawafanya watoto wao wakienda huko wahangaike sana kwa kukosa kazi. Mwishowe, wengine wao wanajiingiza katika dawa za kulevya na baadhi yao kuwa wendawazimu.

### 4.6 Mapenzi

Visa vya wazazi wanaoathirika kisaikolojia kutokana na changamoto za kimaisha vinaendelea kuongezeka kila uchao. Kulingana na Gopfert na wengine (2004) na O’Connor (2015), ni vigumu kuishi na mzazi wa aina hiyo kwani yeye husema na kufanya mambo yanayowaudhi au kuwakanganya watoto. Hii ni kwa sababu watoto wengi hugundua kuwa wazazi hao hawachezi, kuzungumza wala kutalii sehemu mbalimbali na watoto wao. Ni katika hali hii ambapo

tunamkuta mwanamume Ndi- baada ya kupoteza kazi yake. Anajitenga na wanafamilia yake kabisa. Mwanamume huyu anashindwa kutekeleza majukumu yake katika jamii hivyo, hadhi aliyokuwa akipewa hapo awali inapungua au kupotea (Otite, 1994). Kutokana na mabadiliko hayo, tunaona maudhui ya mapenzi yakijitokeza kupitia bintiye Kilua. Ndi- anapofutwa kazi na kuathirika kisaikolojia, Kilua yu mstari wa mbele kumtembelea chumbani alimojifungia, kummalizia upweke na kumjulia hali baada ya Ndi- kujitenga na kila mtu. Anamweleza babake:

> Mimi nataka kuwa karibu na wewe kama zamani. Nataka kuzungumza na kucheza na wewe kama zamani (Uk. 60).

Kilua alimpenda sana babake ndiyo sababu, aliathirika sana kutokana na kujitenga kwa babake. Zaidi ya hayo alimtetea babake kwa ujasiri dhidi ya wanafunzi wenzake walipomweleza kuwa babake alikuwa na wazimu:

> Watoto wananichokoza skuli…Ati, kweli baba unapita ukivua…Tayari alikuwa ameathirika vibaya. Nilimhisi akiungulika na kujikunjakunja na kujipalilia kama pweza aliyetupwa juu ya makaa ya moto. Uso wake ulikuwa umekunywa huzuni na madhehebu ya kitoto. Machozi yakamfumuka na kumlengalenga machoni (Uk. 90-91).

Kwa kawaida mtoto ampendaye mzazi wake huhisi vibaya sana akisikia watu huko nje wakimpiga vijembe mzaziwe. Hata kama mambo yanayozungumzwa ni ya kweli, mtoto bado huhisi vibaya. Kwa namna yoyote ile atajaribu kumtetea na kumsifu mzazi (O’ Connor, 2015)

Mapenzi ya Kilua kwa babake yalifika kilele tunapomwona akimpangusa babake machozi na pia kumpelekea sehemu ya chakula chake.

> Tulitazamana na nadhani machozi yalikuwa yakinitoka, maana Kilua, kama aliyefundishwa, alipeleka vidole vyake na kunifuta umajimaji mashavuni (Uk. 60).

Vile vile, tunaelezwa kuwa;

> Mama anasema… Anasema mama… anasema kuwa unakigomea chakula chetu bure. Hakika neno. Si chakula cha ukahaba ! Na hiki ninachokuwekea ni changu mimi. Nilipopewa nilikigawa kwa siri sehemu mbili. Moja yako, moja yangu (Uk.57).

Ndi- alikuwa amekisusia chakula cha mkewe Bi M kwa kudhani kuwa mkewe anashiriki ukahaba ili apate pesa. Kilua anaonyesha mapenzi yake kwa babake kwa kumfahamisha kuwa mamake alikuwa akifanya kazi halali na kupata pesa za kununua chakula. Japo Kilua ni mdogo kwa umri, busara na mapenzi yake kwa babake yanajitokeza. Anaonekana kuelewa machungu apitiayo babake baada ya kufutwa kazi. Anakuwa pale kumhimiza na kumtia moyo.

Mtima, bintiye Ndi- aliyekwenda Uingereza kutafuta kazi, pia anadhihirisha mapenzi mengi. Anapotambua kuwa babake amejawa na upweke baada ya kufutwa kazi na kujitenga na watu, anaamua kumnunulia tarakilishi ili waweze kuwasiliana kupitia barua pepe. Anamweleza :

> Zawadi ndogo dhaifu, lakini kubwa najua. Mwenzako huyu kompyuta atakuwa. Kwenye upweke wako uliouchagua. Katika watu wote duniani, mimi ndiye ninayekutambua vilivyo (Uk. 7).

Inadhihirika kuwa mshahara wa kwanza wa Mtima ndio ulionunua tarakilishi hiyo. Haya ni mapenzi makuu sana ya binti kwa babake. Kila mara alimjulia hali na hata kumwondolea upweke kwa kumfahamisha mengi kuhusu Uingereza.

### 4.7 Nafasi mpya ya mwanamke

Frimpong (2012), alifanya utafiti kuhusu wanawake katika karne ya ishirini na moja. Kwanza anarejelea nafasi yao hapo awali. Anabaini kuwa, katika bara la Afrika wanawake walionekana kama viumbe vya kuhifadhi boma na pia kuzaa. Huko Uropa, wanawake walidhaminiwa kutegemea nafasi za wazazi wao katika jamii. Kule Uchina walipatikana katika fikira tu. Pia hawakuruhusiwa kufanya kazi katika viwanda au hata kurithi mali. Hata hivyo, karne ya ishirini

na moja imekuja na mabadiliko mengi. Huko Uchina, Chama cha Ujamaa kiliinua na kuboresha maisha ya wanawake. Kiliwakomboa kutoka kazi za nyumbani na kuwapa kazi viwandani. Huku Afrika, imani kuwa kumwelimisha mtoto wa kike ni kupoteza pesa ilianza kubadilika hasa mwisho wa karne ya ishirini. Huko Uropa, wanawake walianza kupigania usawa wa jinsia.

Hapa nchini Kenya, utafiti wa Aluanga (2013) unatueleza kuwa mwaka wa 1974, mwanamke mmoja kwa jina Julia Ojiambo aliweka historia kwa kuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa Waziri Msaidizi. Hivi leo wanawake hawajaachwa nyuma katika masuala ya siasa kwani wanashikilia nyadhifa mbalimbali serikalini kama wabunge, mawaziri na kadhalika. Anataja wanawake waliojulikana kwa mchango wao wakiwemo Bi. Martha Karua, Bi. Charity Ngilu, Bi. Beth Mugo, marehemu Prof. Wangari Maathai na kadhalika.

Kupitia mabadiliko haya yote, ni wazi kuwa mwanamke katika karne ya ishirini na moja yu huru na anafanya kazi nzuri za kupata faida au kulipwa mshahara. Kando na hayo, kiwango chake cha elimu kimeongezeka.

Vivyo hivyo, katika riwaya ya *Dunia Yao*, kutokana na mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume, nafasi mpya ya mwanamke imejitokeza. Mwanamke ni mkakamavu na mwenye bidii. Baada ya Ndi-, mumewe Bi. M kufutwa kazi, mwanamke huyu hakuungana na mume wake kuomboleza na kuathirika daima. Tunamwona akianzisha biashara ya kuuza vyakula ofisini. Kwa namna hii, anaikimu familia yake hasa upande wa lishe kutokana na fedha apatazo. Aidha baada ya Yungi kubadilika kitabia na kuacha uasherati, anajikakamua na kufanya biashara tofauti tofauti. Kutokana na fedha anazopata, Yungi ananunua vifaa vya nyumbani ambavyo Jitu, kakake, anauza. Tunaelezwa :

> Si kazi moja wala mbili. Mara kafuma foronya na kuziuza. Mara kazitia nywele za wenzake katika chombo fulani na kuzitokosa…kisha akawatoza pesa. Mara kasafiri na kurudi na mabunda ya mitumba na kwa muda wa wiki kadhaa na mbele ya mlango wetu palikuwa na duka la nguo hizo kuukuu. Pesa zikaingia mikononi mwake. Taratibu alianza kununua vifaa vya nyumba, angalau vile muhimu tulivyovipoteza (Uk. 151).

Ikumbukwe kuwa wakati wanawake hawa walikuwa wanafanya kazi hizo, Ndi- alikuwa nyumbani tu bila hata ya ishara ya kutafuta au kuanzisha biashara yoyote angalau aikimu familia yake. Badala yake, mkewe na bintiye ndio wanaikimu familia hiyo. Kinyume na babake, Yungi hakati tamaa maishani. Licha ya kushindwa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya ukosefu wa karo, anatafuta namna nyingine ya kufaulu maishani. Kwa namna hiyo, mwanamke anaonekana kuwa ni mtu mwenye busara. Kilua pia anadhihirisha busara anapokuwa akimweleza babake jinsi wenzake shule wanasema kuwa Ndi- ana wazimu. Anamwambia :

> Wendawazimu ni wao. Hawajui kwamba huna mshahara tena. Huna nguvu tena. Huna tegemeo tena. Huwezi kutuendesha. Nani asiyeingiwa na wazimu katika hali kama hiyo ? (Uk 91)

Kilua alikuwa na busara ya kuweza kuelewa athari za kupoteza kazi hasa kwa mwanamume. Alielewa fika kuwa mwanamume akishindwa kuikimu familia yake, ni aibu sana. Anaonekana bure na haya yote yanaweza kumwathiri kisaikolojia. Mwisho, kupitia kwa Yungi mwanamke anajitokeza kama mpiganiaji haki za umma. Mwishoni mwa riwaya yeye yu katika harakati za kupinga mipango ya kuvunja nyumba za eneo lao kwa kujenga hoteli ya Wataliano. Bi. M anamfahamisha Ndi- :

> Yungi amekwenda mkutanoni…Si unajua kwamba wanataka kuvunja nyumba za eneo letu hili lote kwa kujenga hoteli ya Wataliana ? Tumeshaunda umoja wa kupinga na kukataa. Yungi amechaguliwa kuwa kiongozi na kwa hivyo yumo mbioni, kukutana na wakaazi. Siku hizi hana nafasi. Kazi zinamtaka. Kugombania haki kunamngoja (Uk.210).

Vile vile, watoto wa kike katika riwaya ya *Dunia Yao* wanapewa nafasi ya kusoma sawa na wale wa kiume na hata wanafika vyuo vikuu kwa mfano Mtima. Hii ni tofauti na Maimuna katika *Utengano* ambaye haruhusiwi kwenda shuleni kama kakake Mussa.

Al-Baker na Al-Sher'ah (2000), waligundua kuwa katika jamii za kisasa za Waarabu na Saudia ; mamlaka ya kina baba yamepungua na kukosa nguvu ikilinganishwa na miaka ya awali. Kwa upande mwingine, mamlaka ya kina mama yameongezeka kutokana na elimu ya kina mama na watoto wao. Kupata amali na tamaduni geni kunawapa motisha wa kuhoji na kudadisi sheria jadi kuhusu familia. Mambo haya pia yanadhihirika katika riwaya teule hasa kupitia Yungi anapomweleza baba yake kuwa ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume.

**4.8 Kutengana na kusambaratika kwa familia**

Kama ilivyokwisha tajwa, kutokana na tafiti mbalimbali, mwanamume anaposhindwa kutekeleza jukumu lake la kukimu familia yake ; yeye huona aibu na kujitenga kabisa na watu. Aidha, kutokana na utafiti wake, Lamb (2004) anatambua ya kwamba baba huathiri watoto wake kwa namna sawa na afanyavyo mama. Hii ni kupitia kuwaunga watoto kimawazo, kuwahakikishia usalama na uwepo wao katika maisha ya watoto hao. Baba asiyekuwepo au asiyejihusisha na watoto wake husababisha athari nyingi mfano utengano na watoto kujihisi duni.

Inaonekana katika riwaya ya *Dunia Yao* kuwa, nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume unapobadilika, utengano huanza kujitokeza. Mwanaume anaposhindwa kuikimu familia yake anajihisi kuwa hana maana. Hivyo, anajitenga na watu akiwemo mkewe. Kwa miaka mitano, Ndi- alikuwa hajaonana na mkewe kimwili kwani Bi. M alikuwa akitoka nyumbani alfajiri na kurejea magharibi. Naye Ndi- alikuwa akitoka chumbani mwake jioni na kurejea usiku wa manane. Anasema :

> Ni kweli alivyosema Kilua, mimi na mamake hatujaonana muda mrefu, ingawa bado tu mke na mume ndani ya nyumba moja (Uk. 90).

Aidha, Mtima bintiye Ndi- anatengana na familia yake anapoenda Uingereza kutafuta kazi. Vile vile Dubwa, kifungua mimba wa Ndi- anajitenga kabisa na familia yake. Mwishowe familia inasambaratika tunapoona jinsi ukatili unamwingia Jitu na anambaka Kilua na kumwua kisha Jitu mwenyewe anauawa.

Vile vile, bwana Ndera anaposhindwa kukimu na kuidhibiti familia yake, utengano unatokea. Watoto wake wawili wanajiingiza katika ulevi na kuishia jela ya wendawazimu. Mwingine anafungwa jela kwa wizi. Kuhusu mkewe, tunaelezwa :

> Kubwa zaidi, mkewe Masika, au kwa jina maarufu Kisura, kamkimbia. Kachupia farasi mwenye soji jema kwenda ng’ambu nyingine ya uchumi (Uk. 129).

Mifano hiyo yote inaonyesha wazi kuwa mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wanaume yana athari kubwa sana kwa familia. Mwanamume akishindwa kuikimu na kudhibiti familia yake utengano huingia kati na hatima yake ni kusambaratika kabisa kwa familia. Watoto wanapokosa baba wa kuwaelekeza, kuwashauri na kuwaadhibu wanapofanya makosa, wanakosa umoja na mshikamano kama ndugu na kila wakati kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe katika familia. Huruma kwa ndugu zao inakwisha kabisa na nafasi yake kuchukuliwa na ubinafsi na ukatili mwingi. Kando na hayo, wanakuwa kama windo kwa kila nguvu ijayo upande wao kwa mfano utandawazi. Aidha, wanashinikizwa na wenzao kufanya lolote lile hata likiwa baya. Wanashiriki uhalifu na wengine wanaishia jela. Zaidi ya hayo, wanashinikizwa kushiriki ulevi wa dawa na baadhi yao wanaishia kuwa wendawazimu. Kwa upande mwingine, wanawake nao wanakumbwa na upweke wa hali ya juu kwani wanaume wao hawajishughulishi nao. Baadhi yao

wanatorokea waume wengine wanaoweza kuwakimu maishani. Familia zinaposambaratika, jamii nzima inaingiwa na udhaifu kwani familia thabiti ndiyo nguzo ya jamii thabiti.

### 4.9 Utandawazi na athari zake

Ni kutokana na mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume ambapo tunamulikiwa athari za utandawazi kwa jamii za Afrika. Mwandishi alidhamiria kutufahamisha kuhusu uwepo wa utandawazi katika karne ya ishirini na moja kwa kuangazia faida na hasara zake. Hata hivyo katika riwaya ya *Dunia Yao*, mfumo wa utandawazi umepewa sifa ya unajisi. Ni asilimia ndogo sana inayoonyesha umuhimu wake katika jamii za Afrika. Kwa namna hii, mwandishi alinuia kututahadharisha dhidi ya utandawazi kwani kwa kiasi kikubwa haumfaidi Mwafrika. Sehemu ya maisha ya jamii, iliyoathiriwa zaidi na utandawazi ni utamaduni (Mwirabua, 2014). Kulingana na Mishra (2004) aliyeangazia utafiti uliofanywa mjini Washington, utandawazi unaoendelea unanuia kuleta utamaduni mmoja ulimwenguni mzima. Utandawazi unalenga kulazimisha utamaduni wa Amerika kila pahali duniani. Ndi- anasema:

> Utamaduni tusioutaka hatuwezi kuuzuia tena. Unakuja kwa mawimbi yenye nguvu. Ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi ya kuchekesha…Na miili yetu inajazwa sumu. Nyama ya ng’ombe, kuku, kondoo, nafaka, mbogamboga zinatisha kuliwa…. tazama vyombo vya habari na mawasiliano vinavyosambaza uhalifu, uwongo na unafiki…. michezo ya kikatili wanayoiona vijana kwenye video, DVD na sinema. Si bunduki, si silaha zinazoundwa na kuuzwa…Huu ndio upeo wa dunia ya leo. Dunia Yao (Uk. 49).

Ni dhahiri kuwa mfumo wa utandawazi umeathiri pakubwa sehemu zote za utamaduni wa Mwafrika kama vile mavazi, hulka, lishe, vyombo vya mawasiliano na kadhalika. La kushangaza ni kuwa Waafrika wengi hasa vijana wanaiga kila kitu kinacholetwa na mfumo wa utandawazi. Hawachunguzi na kung’amua kuwa si kila kitu kitokacho uzunguni ni chema cha kuigwa. Katika

kuiga raha za uzunguni kama vile dawa za kulevya, vijana wengi wameathirika kiafya na kuwa watu ovyo wasioweza kuchangia katika ustawi wa nchi zao.

Aidha, vijana wengi wanaiga tabia wanazoona katika vipindi au sinema za wazungu kwenye televisheni au mtandao. Matokeo yake ni mauaji na kushiriki ngono ovyo ovyo. Waafrika wengi hasa vijana wamewacha kudhamini maadili mema ya Kiafrika waliofunzwa na au kujifunza kutoka kwa wanajamii wengine. Badala yake, wanaonea fahari utamaduni wa kigeni ulioletwa na mfumo wa utawandazi. Yetu si yetu tena, ya wenzetu ndiyo tunayoyafanya yetu. Hii inasababisha migogoro isiyokwisha kati ya vijana na wazee. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, tunamwona Yungi akidhubutu kumwambia babake hivi:

> Fungua macho…majirani wote wanawaachia watoto wao wa kike na wa kiume wafanye wanavyopenda siku hizi. Wewe bado unang'ang'ania ukale. Wewe bado unataka kukamata na kudhibiti. Unataka uongozi usiouweza. Huwezi tena kutuendesha (Uk.25).

Kauli hii inamuumiza sana Ndi- ila hajibu chochote. Tunaonyeshwa mawazo yake kama ifuatavyo:

> Lakini nilijua ni vigumu kwa vijana kufahamu hatari iliyomo ndani ya usasa wanaoutaka. Na wao hawalaumiki, ukitazama kasi ya mambo ya usasa na utandawazi inavyosonga. Yetu si yetu tena, ya wenzetu ndiyo tunayoyafanya yetu. Tukitaka tusitake. Mabaya au mazuri! (Uk.26)

Siraji (2007), analaumu teknolojia mpya kwani huchangia kuongeza utengano katika familia. Hii ni kwa sababu watu hawatengi muda wa kutosha wa kuzungumza na kujadiliana kama familia. Jambo hili linadhihirika katika riwaya ya *Dunia Yao* hasa Ndi- alipotumia muda mwingi katika tarakilishi huku akijitenga na mkewe na watoto.

Fauka ya hayo, utandawazi unachangia pakubwa kuendeleza dhuluma na unyanyasaji kwa Mwafrika. Vyombo vya habari havina ari na uchungu katika kuchagua na kupanga habari zilizo na maslahi ya Waafrika. Teknolojia ya habari na mawasiliano imetumiwa na wakoloni kuendeleza utamaduni wao huku Afrika. Mwafrika hufanywa kuchukia kilicho chake na kupenda kila kilicho kigeni. Kwa namna fulani huu ni ukoloni mamboleo.

Kwa upande mwingine faida ya utandawazi imejitokeza. Ndi- anapojitenga na familia yake na kujifungia chumbani baada ya kufutwa kazi, anawasiliana na bintiye Mtima kupitia barua pepe kwa tarakilishi. Mtima anamfahamisha mengi kuhusu safari yake kuelekea Uingereza na maisha yake baada ya kufika huko hasa jinsi alihangaika kutafuta kazi. Kupitia kwa barua pepe zao tunajuzwa mengi kuhusu ubinafsi uliowajaa wazungu wengi ambapo kila mtu anaijali nafsi yake pekee.

Kwa ufupi basi mfumo wa utandawazi unasaidia katika usambazaji na uenezaji wa habari kote ulimwenguni kwa urahisi. Baadhi ya habari hizi kwa namna fulani zinakuwa za manufaa katika kustawisha nchi. Kwa mfano, mashine za kisasa zinazotumika katika viwanda mbalimbali zinasaidia kuongeza bidhaa zinazoweza kuuzwa na hivyo kukuza uchumi wa nchi.

## 4.10 HITIMISHO

Katika sura hii tumeangazia kwa kina athari za mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui. Maudhui yaliyojitokeza ni kama vile mmomonyoko wa maadili, mapenzi, malezi, kukita mizizi kwa ukoloni mamboleo, ukosefu wa kazi, athari za utandawazi na mengineyo. Imedhihirika kuwa wahusika katika kazi ya fasihi wakibadilika kwa namna yoyote ile, kunakuwa na athari kubwa upande wa maudhui. Maudhui mapya pia yanaibuka na kutusaidia kuelewa zaidi dhamira ya mwandishi

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari wa utafiti huu. Pia, malengo ya utafiti yameelezwa pamoja na yaliyomo katika kila sura. Fauka ya hayo, matokeo ya utafiti yamefafanuliwa kwa kina kwa kuonyesha namna utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo yake huku tukioanisha na mihimili teule ya nadharia. Vile vile, matatizo au changamoto zilizopitiwa na mtafiti zimeelezwa, mchango wa utafiti ukafafanuliwa na mwisho mapendekezo ya tafiti za baadaye yakaelezwa.

### 5.1 Muhtasari

Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu. Kwanza kabisa, ulidhamiria kuonyesha mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume kama yalivyodhihirika katika riwaya mbili teule za Said A. Mohamed: *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006). Lengo lingine lilikuwa kuonyesha sababu za mabadiliko hayo. Mwisho, utafiti huu ulidhamiria kubainisha athari za mabadiliko hayo katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui.

Ili kufikia au kutimiza malengo hayo, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii ina mihimili kadhaa lakini ni minne pekee ambayo ilitumiwa kuelekeza utafiti huu. Mwanzo, katika fasihi, uhalisia hujihusisha na uwezo wa kuchora au kusawiri hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Pia, huonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji hukumbana nao. Aidha, mielekeo ya jamii haipingani na historia ya wakati wake na hii ina maana kuwa maswala mbali mbali ya kijamii ikiwemo fasihi huelekezwa na matukio

yatendekayo kwenye jamii kwa wakati fulani. Mwisho, msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Ya kwanza iliangazia mahitaji ya kimsingi katika kila utafiti kwa mfano usuli, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na hatimaye mbinu za utafiti. Nayo sura ya pili ilionyesha mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya teule. Katika sura ya tatu, tuliangazia sababu za mabadiliko hayo na kwenye sura ya nne, tulishughulikia athari za mabadiliko hayo katika uendelezaji wa riwaya kimaudhui. Hatimaye, sura ya tano imetoa muhtasari wa utafiti, matokeo na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

**5.2 Matokeo**

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa kuna mabadiliko mengi ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume hasa katika karne hii ya ishirini na moja. Hapo awali, lilikuwa ni jukumu la mwanamme kutafuta riziki na kukimu familia yake kwa jumla. Jamii nyingi za kiafrika zilijikita kwenye mfumo wa kuumeni ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanamme katika nyanja zote za maisha (Wamitila, 2003). Mwanamume ndiye alikuwa kiongozi wa familia hivyo, alikuwa na uwezo mwingi juu ya mwanamke na watoto. Naye mwanamke alikuwa na wajibu wa kuzaa, kuwalea watoto na kupika.

Hata hivyo, katika karne ya ishirini na moja mabadiliko makuu yameshuhudiwa katika asasi hii ya ndoa. Nafasi ya mwanamume ya kutafuta riziki na kukimu familia imemponyoka na kuchukuliwa na jinsia ya kike. Hii imesababishwa na mabadiliko yaliyodhihirika katika jamii. Ukweli usiopingika ni kwamba ugumu wa maisha kiuchumi hamruhusu mke wa sasa kukaa tu

nyumbani huku akimngoja mume kumkimu na kumridhisha kwa kila jambo. Aidha, kutokana na wanawake kufaidi elimu wanaweza sasa kupata ajira zinazowapa pesa. Hadhi yao kiuchumi imeanza kuimarika na wanaweza kukimu familia kama wanaume au bora zaidi. Kando na hayo, kumekuwa na nguvu za utandawazi ulimwenguni zilizoathiri sekta zote ikiwemo ndoa. Tamaduni za magharibi ambapo hata wanawake hukimu familia zao sawa na wanaume, zimesambazwa katika bara la Afrika na kukumbatiwa na Waafrika. Mwanamke anachukuliwa sawa na mwanamme hivyo anaweza kufanya ayafanyayo mwanamme.

Haya yanaoana vyema na mhimili wa nadharia ya uhalisia usemao kuwa uhalisia una mashiko katika hali halisi. Kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii, inasawiri matukio yanayoshuhudiwa katika ulimwengu au jamii halisi. Hii ni kwa sababu, watunzi hujishughulisha na utunzi kufuatana na mkondo wa wakati na mabadiliko ya wakati. Ndiposa mhusika Ndi- anapopoteza kazi yake na kutoonekana kujishughulisha kutafuta nyingine au kuanzisha bishara ili kuikimu familia yake; mke wake kwa jina Bi. M anajitwika jukumu la kutafutia aila yake riziki. Pia, binti yao Yungi, anaonekana kuchangia katika ununuzi wa vifaa vya nyumbani. Ukweli huu unamuuma sana Ndi- na ndio maana anasusia chakula kwani anakumbwa na aibu nyingi na kuhisi kuwa ni jukumu lake kama mume kuitafutia aila yake riziki. Kwa kutokubali jambo hili, anawaza kuwa chakula hicho kilikuwa cha ukahaba. Vile vile, kutokana na aibu nyingi ya kushindwa kukimu familia yake, Ndi- anajitenga na aila yake na kujifungia chumbani siku kutwa. Pia, iwapo ameenda barazani kwa wazee wenzake, anaondoka jioni na kurejea usiku wa manane wakati familia yake ishalala kwani anaona aibu. Matendo hayo yanadhihirisha hali yake ya kisaikolojia kulingana na mhimili mmojawapo wa nadharia ya uhalisia.

Mabadiliko mengine yaliyoonekana katika nafasi ya wahusika wanaume ni kuwa, karne ya sasa mwanamume ameshindwa kutunga sheria na pia ameshindwa kudhibiti familia yake. Katika

miaka ya awali, kulingana na mfumo wa kuumeni katika jamii za Kiafrika, mwanamume alitarajiwa kuwa mtawala katika familia. Mke na watoto walikuwa chini ya uongozi wake na walipaswa kutii sheria zote alizotunga. Mwanamume alikuwa pia mkali na wa kuogopwa. Ndio maana katika riwaya ya *Utengano*, Bi. Tamima anaposhikwa na uchungu wa uzazi hathubutu kuvunja sheria za mumewe Bw. Maksuudi aliyekuwa amekanya dhidi ya kutoka nje ya kasri. Bi. Tamima alikuwa tayari kupoteza maisha yake mradi asiende kinyume na sheria hiyo. Kinyume kinadhihirika katika karne ya ishirini na moja ambapo, kutokana na kusambazwa kwa dhana mpya za kimagharibi kupitia utandawazi, mambo yamebadilika.

Dhana hizo ni kama vile mwanamke ana haki sawa na mwanamme. Basi, wanawake na wasichana wamefanywa kupigania haki za usawa na hawako radhi kuendelea kunyenyekea na kutii sheria au kuwa chini ya uongozi wa mwanamume. Watoto nao hawakuachwa nyuma. Kupitia utandawazi, wamefanywa kuamini kuwa wanaweza kujiamulia mambo yote na pia kufanya watakayo kwani ni haki yao na kuna demokrasia. Nguvu hizo za utandawazi zimeathiri sana ndoa na familia kwa jumla na kusababisha mmomonyoko wa kimaadili. Watoto na vijana wanawakosea adabu wakubwa wao na kuwa na mienendo iliyopotoka mfano, kushiriki ulevi, ngono za kiholelaholela, wizi, ubakaji kati ya maovu mengine. Hata watoto wa kike wanachelewa kurudi nyumbani. Tunamwona Yungi akirejea usiku wa manane akiwa mlevi chakari. Inawawia vigumu wanaume kuweza kudhibiti wanawake na hata watoto wao hivi kwamba wanabaki kutazama tu huku wakiwa wamejaa uchungu na mshangao moyoni.

Kinyume na ilivyokuwa miaka ya awali ambapo watoto waliwazungumzia wazazi kwa heshima, katika karne hii ya ishirini na moja moja watoto wanawaropokea wazazi wao ovyo. Ndiposa Yungi anamwambia babake kuwa sasa watoto watawaendesha wazazi wao.

Fauka ya hayo, imedhihirika kuwa badala ya mwanamume katika karne hii kutafuta suluhisho la matatizo yeye hukata tamaa upesi. Hii ni kinyume na matarajio ya mfumo wa kuumeni ambapo wanaume walitarajiwa kuwa wakakamavu na wasiodhihirisha hisia zozote za unyonge hata wakati wa matatizo. Licha ya changamoto zozote ambazo zingewakumba, wanaume walitarajiwa kukabiliana nazo kwa uhodari.

Mwanamume hakutarajiwa kulia au kuonyesha hisia zozote za unyonge hata walipokumbwa na vifo vya wapendwa wao. Hivyo, inashangaza kuwaona wanaume katika karne ya ishirini na moja wakidhihirisha unyonge na hata kulia wanapokumbwa na matatizo. Sakarati na Ndi- katika riwaya ya *Dunia Yao* wanaomboleza hali yao ya kupoteza kazi inayowafanya kushindwa kukimu familia zao. Badala ya kutafuta kazi mbadala au hata kuanzisha biashara za kuwawezesha kukimu familia zao, wanakata tamaa. Ndi- anajifungia chumbani siku nzima na kujihurumia. Kwa namna hii wanashindwa hata kuendelea kuwaelimisha watoto wao na watoto hao wanaathirika sana baadaye. Hatimaye kujitenga huku kunaathiri ndoa na familia ya Ndi- kwani inaelekea kusambaratika.

Mwisho, mwanamume katika karne ya ishirini na moja anajihusisha na kazi za nyumbani kwa mfano ulezi wa watoto. Hii ni tofauti kabisa na miaka ya awali ambapo ulezi wa watoto na kazi za nyumbani zilihusishwa na jinsia ya kike pekee. Naye mume alijihusisha na kwenda kutafuta riziki na kufanya kazi za nje. Mwanamume wa sasa anawachiwa watoto wadogo ili awatunze na hata kuwalisha wakati ambapo mke wake amekwenda kutafuta riziki. Tunamwona Ndi- akiwachiwa kitoto chao cha miezi mitatu ili akitunze wakati mke wake kwa jina Bi. M, anapokwenda kuuza vyakula ofisini ili aila yake ipate riziki. Aidha, Ndi- anaamshwa siku nyingi ili asaidie katika kazi za nyumbani kama vile kufagia, kusafisha msalani, kufua nguo na pia kupiga pasi. Wakati huo binti yao Yungi yu mkutanoni kwani alikuwa amechaguliwa kuwa

kiongozi wa kutetea haki za wanakijiji dhidi ya kubomolewa nyumba na Wataliano. Haya ni mabadiliko makubwa ambapo kazi za nje na zilizotengewa jinsia ya kiume zinatekelezwa na jinsia ya kike katika karne ya ishirini na moja. Haya ndiyo mabadiliko yanayoshuhudiwa katika jamii ya sasa na ndiposa yanaangaziwa kwenye fasihi kwani kulingana na mhimili mmojawapo wa nadharia ya uhalisia, mielekeo ya jamii haipingani na historia ya wakati wake.

Kando na mabadiliko ya nafasi, utafiti huu pia uliangazia mabadiliko ya mtazamo wa wahusika wanaume. Kwanza, ulitafiti mtazamo kuhusu uhuru wa mwanamke. Utafiti ulidhihirisha kuwa katika miaka ya awali, mwanamume alimnyima mwanamke uhuru wa kutoka nje na kutangamana na mazingira, wa kutoa maoni yake kuhusu masuala tofauti tofauti na hata wa kushikilia nyadhifa za uongozi. Aidha, mwanamume alimwamulia mwanamke kila kitu hata kuhusu elimu ambapo hakumwelimisha mototo wa kike kufikia viwango sawa na mtoto wa kiume. Sababu mojawapo ni kuwa, hakumwonea hadhi mwanamke na pia aliona kuwa mwanamke hafai kupewa uhuru ili asipotoke kimaaadili au aanze kumtawala mwanamme.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mwanamume anaonekana kumpa mwanamke uhuru wa aina fulani. Pia, anauheshimu uamuzi wa mwanamke. Wakati Mtima anapoamua kwenda Uingereza, Ndi-, babake, hampingi wala kumzuia. Anasema kuwa ameshakuwa mkubwa wa kuiendesha nafsi yake ndani ya dunia yake. Vile vile, Yungi anaporejea usiku Ndi- anasema kuwa ana uhuru wa kuyaendesha maisha yake. Mwanamume amemwacha mwanamke ajiamulie atakayo. Sababu mojawapo ya jambo hili ni kutokana na mabadiliko ya kijamii hasa kutokana na athari za utandawazi. Dhana za demokrasia zimekumbatiwa ambapo mwanamke ana haki sawa na mwanamme. Nguvu za utandawazi zimefifisha tamaduni za kiafrika kwa mfano utaratibu wa jamii kulingana na mfumo wa kuumeni. Vile vile, mtafiti ana maoni kuwa kutokana na mabadiliko ya kijamii kuhusiana na elimu ya wanawake, mwanamme ameona kuwa kuendelea

kushikilia mila na tamaduni zilizopitwa na wakati hakuna faida. Katika kumwelimisha mtoto wa kike hadi viwango vya juu, mwanamume amedhihirisha kuwa mtoto wa kike ni sawa na wa kiume hivyo anapaswa kupewa nafasi sawa ya elimu kwani ni muhimu sana katika karne ya sasa.

Vile vile, mtazamo wa mwanamume kuhusu ukwasi na madaraka umebadilika. Katika riwaya ya *Utengano*, mhusika mkuu Maksuudi anaamini kutumia mbinu yoyote ile ili kupata chochote anachotaka. Hii inamaanisha kuwa mwanamume alikuwa radhi hata kuwakandamiza wengine ili akidhi mahitaji yake. Ndiposa anashiriki ufisadi na biashara ya magendo bila kujali mradi apate ukwasi mwingi. Pia, anatumia unafiki na ahadi nyingi za uongo ili achaguliwe kama kiongozi na anapokwisha kuchaguliwa anaanza kunyakua mali ya umma.

Hata hivyo, katika karne ya ishirini na moja, kupitia mhusika mkuu Ndi- inabainika wazi kuwa wanaume wengi wana mtazamo hasi kuhusiana na tabia ya kuwakandamiza wengine ili wapate ukwasi na mali. Anasema kuwa hajawahi kukanyaga na kusagasaga watu kwa nguvu za kipawa chake. Zaidi ya hayo, anabaini ya kwamba hajawahi kuota kuwa na ukwasi na kiburi kwani vitu hivi huangamiza nafsi ya mtu na za wengine. Msimamo wake dhabiti dhidi ya kudhulumu umma kwa nia ya kujitajirisha unaonekana pale anapokataa kushirikiana na wenzake kazini katika ufisadi na mipango isiyofaa umma maskini kwa lolote. Ndiposa anafutwa kazi.

Hatimaye, mtazamo wa wanaume kuhusu kazi na malipo halali unaonekana kubadilika hasa kupitia mhusika mkuu Ndi- katika riwaya ya *Dunia Yao*. Anaonekana kuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kazi ambazo zitamfanya mtu ashiriki maovu au kupata malipo yasiyo halali. Kwake, kazi nzuri si ile inayompa mtu mshahara mkubwa na kumfanya awakalie wenzake bali kazi njema ni inayodumisha heshima kwako na kwa wengine. Ni kazi ya furaha kwako na kwa wengine. Ndiposa anachukia kazi ya utawala kwani kwake yeye, hii ni kazi ya ukorofi.

Anawafunza wasomi kuzingatia maadili mema katika kutafuta kazi ili iwe ya faida kwako na kwa wengine na pia iwe kazi yenye mapato halali.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti ana maoni kuwa kutokana na ugumu wa kiuchumi na pia mabadiliko ya kijamii kuhusiana na malezi, elimu ya wanawake na mabadiliko mengine mengi; mwanamume hana budi kubadilisha mtazamo wake. Haina haja kuendelea kushikilia baadhi ya tamaduni za kale ambazo zimepitwa na wakati. Aidha, hamna kosa kwa mwanamke kutafuta kazi au kuanzisha biashara ili asaidie mumewe kukimu familia. Gharama ya maisha imepanda na hivyo hata mwanamke anafaa kusaidia. Vile vile, kuwepo kwa changamoto maishani ni jambo la kawaida na kupoteza au kufutwa kazi ni mojawapo. Si vyema kwa mtu kufa moyo akikumbwa na jambo kama hilo bali, anafaa kujizoazoa na kutafuta kazi nyingine au hata kuanzisha biashara ili kujikimu. Iwapo Ndi- angefanya hivyo, watoto wake wangekamilisha masomo yao na kufanikiwa zaidi maishani.

Jambo lingine ni kuhusiana na utandawazi na athari zake katika jamii hasa za Kiafrika. Mtafiti ana maoni kuwa, ingawa kulingana na riwaya teule utandawazi umesawiriwa kama nguvu zisizoepukika katika karne ya ishirini na moja ; ni vyema wazazi wawe chonjo. Japokuwa watoto na vijana katika karne hii wameonekana kutia nta masikioni kuhusiana na ushauri wa wakubwa, wazazi wasife moyo. Wanaume wasikimye na kuacha watoto na vijana waangamie katika athari hasi za utawandazi. Wanafaa kujaribu wawezavyo kuwafungua macho watoto na vijana ili wajue kuwa si mambo yote ya uzunguni yanafaa kukumbatiwa na kuigwa. Wanafaa kufunzwa kuchuja ili wachague yaliyo mema na kukataa mabaya. Kulingana na mhimili wa mwisho wa nadharia ya uhalisia, msanii huangazia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Hivyo, imedhihirika wazi kuwa utandawazi umeathiri jamii nyingi za Kiafrika na kutufanya kama tusio na mwelekeo.

Hivyo, tunafaa kupevuka ili kupokea yaliyo mema kuhusiana na utandawazi huku tukikataa kabisa yaliyo ya kupotosha na kuangamiza.

### 5.3 Mchango wa utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi na hata waandishi wa fasihi. Wanaume watafaidika kwa kuwa watagundua kuwa mabadiliko ndicho kitu cha kudumu maishani. Hivyo, ikiwa mabadiliko yana manufaa hayafai kukataliwa. Aidha, si vyema wanaume kufa moyo wakikumbwa na changamoto. Pia, wasomi kama vile vijana watafaidika kwani wataanza kutathmini na kupima mambo mageni kabla ya kuyakubali au kuyakataa. Watafiti wa fasihi nao watafaidi maarifa mapya kutokana na utafiti huu.

### 5.4 Changamoto

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadhaa hasa ukosefu wa vitabu vya Kiswahili vya kusomwa. Ilimbidi mtafiti asome vitabu na makala mengi yaliyoandikwa kwa lugha ya Kingereza kisha akatafsiri kwa Kiswahili. Wakati mwingine, ilikuwa vigumu kupata istilahi mwafaka. Vile vile, katika kuufanya utafiti huu mtafiti alikuwa kazini. Aidha, kulikuwa na changamoto ya safari ndefu na gharama kubwa ya kwenda maktabani kufanya utafiti, kupiga chapa na kutolesha nakala. Licha ya hayo, kwa neema ya Mwenyezi Mungu, mtafiti alitia juhudi kubwa ili kufanikisha utafiti huu.

### 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya mbili za Said A. Mohamed : *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006). Utafiti wa kina unaweza kufanywa kuhusu jinsi ya kufahamu vyema athari mbaya za utandawazi. Vile vile,

utafiti mwingine unaweza kuangazia mtazamo wa wanawake kuhusu wanaume katika karne ya ishirini na moja.

**MAREJELEO**


Al-Baker, G. & Al-Sher'ah, H. (2000). The Reality of Parental Authority: An Annalytical Study. *Arab Journal of Education*, 20(1), 18-38

Alsaedy, F. (2015). *Parent-Child Communication: The Impact of Globalisation and Rapid Social Transformation in Khulais- Saudi Arabia*.Queensland University of Technology

Aluanga, L. (2013). The changing face of women leadership over the decades. *Standard Digital* [www.standardmedia.co.ke](www.standardmedia.co.ke) (Accessed on 12th November 2018)

Amadiume, I. (1987). *Male Daughters, Female Husbands: Gender and Sex in an African Society.* London: Zed Publishers Ltd

Ambrose, J. na Palm, S. (2015). Dating in the 21st Century. *The Real Truth Magazine.* The Restored Church of God, Ohio

Appleyard, D. (2007). Househusband backlash as high-flying wives ditch men they wanted to stay at home. *www.dailymail.co.uk/femail/article* (Downloaded on 6th November 2016)

Ayang, S.G. (1970). *A History of Zanzibar*. Nairobi: East Africa Literature Bureau

Bakhtin, M.M. (1986). *The problems of Speech Genres*. Austin. University of Texas Press

Blackstone, A.M. (2003). Gender Roles and Society. *Human Ecology: An Encyclopaedia of Children, Families, Communities and Environments*. Santa Barba Ra. ABC-CLIO

Blunden, A. (1976). *Marx and Engels on Literature and Art*. Moscow: Progress publisher

Cambridge University Press (2008). *Advanced Learners Dictionary 3rd Edition*. Cambridge.Cambridge University Press

Chachage, S. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam. E&D Limited

Chaterji, S. A. (2004). Signs of Change in Patriarchal Ideas about Men and Women's Status and Role in Indian Society. Katika *Gender and Conflict Transformation.*Irenees.net

Chau, R. (2009). Liberalism: A Political Philosophy. *http://www.mannkal.org* (Accessed on 15th April 2017)

Creig, D. (1975) (Ed) *Marxists on Literature*: An Anthology. London. Harmordsworth Penguin Books

Crous, M. L. (2005). *Presentation of Masculinity in a Selection of Male-Authored Post-Apartheid Novels,* University of Stellenbosch.

Dailey, C. (2014). Whats behind the rise of stay-at-home dads? *BBC News Magazine* (Downloaded on 11th November 2018)

Eaton, N. (2011). Study Finds Sex Differences in Mental Illness. *http:www.apa.org* (Downloaded on 18th November 2016)

Flood, M. (1990). "Men Plural." *www.xyonline.net/Menplural/Connell.shtml* (Accessed on 13th October 2016)

Frimpong, Y. (2012). The Woman in the 21st Century And Her Effect On the Society. *https://m.modernghana.com* (Accessed on 13th October 2016)

Gagiano, A. (2000). *Achebe, Head, Marechera: On Power and Change in Africa*.Boulder:Lynne Rienner

Gitau, E. N. (2005). Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume Katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Gopfert, M. et al (eds) (2004). *Parental Psychiatric Disorder- Distressed Parents and Their Families.* Cambridge. Cambridge University Press

Holter, G.H. et al (2009). *Gender Equality and Quality of Life: A Norwegian Perspective* Oslo.Nordic Gender Institute

Harrow, K.W. (1994). *Thresholds of Change in African Literature*.London:Heinemann

Hart, S.M. (2003). Magical Realism in the Americas: Politicalized *Ghosts in one Hundred Years of Solitude, The House of Spirits* and *Beloved*. *Journal of Iberian and Latin American Studies* pp 83-93 (Accessed on 16th November 2016)

Harvey, D. (2003). *The New Imperialism*. Oxford. Oxford University Press

Hill, J. S. (1977). *The Romantic Imagination*. London: Macmillan Press Ltd

Hirsch, E.D. (1967) *Validity in Interpretation*. New Haven&London. Yale University Press

International Labour Office. (2016). *World Employment and Social outlook: Trends* Geneva. International Labour Office

Irele, F.A. (2009). *Introduction: Perspectives on the African Novel*.Cambridge:Cambridge University Press

Kanana, A.S. (2000). Changing the Patriarchal Attitude of Ovawambo Men: Can the Bible help? M.A Thesis.University of Natal,Pietermaritzburg

Kazungu, E.K. (1984). *Utangulizi wa Kina cha Maisha*. Nairobi. Longman Kenya Limited

Kearns, K. (1996). *Nineteenth- Century Literary Realism: Through the Looking Glass.* Cambridge. Cambridge University Press.

Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi. KLB

Kgatia, S.T. (2013). Globalization: Facts and Fictions. *Asian Journal of Social Sciences, Arts and Humanities Vol 1 No. 1*

Khamis, S.A.M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili. Katika: Nathan Ogechi,Naomi Shitemi & Kenneth Simala (eds), *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.*Eldoret: Moi University Press. Pp 3-24

Kimani, W.C. (2003). Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili.Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

King'ei, G.K. (2000: xv) *Miale ya Uzalendo*. Nairobi:Phoenix Publishers

King'ei, G.K. (2002). "Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya." Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press

Kothari, U. (2006). From Colonialism to Development: Reflections of Former Colonial Officers. *Commonwealth & Comparative Politics* vol 44 no.1 pp. 118-136

Lamb, M.E. (2004). *The Role of the Father in Child Development*.E$^{th}$ ed. New York:John Wiley & Son

Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Nineteenth Century Realism*.London;London Macmillan Press

Lawall, S. na Maynard, M. (1984). *The Norton Anthology of World Literature.* London: Norton and Company Ltd

Libby, A. (2012). *Love, Joy, and Feminism: What is Christian Patriarchy?* An Introduction. Patheos

Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism: A sociological survey of writings of Balzac, Stredhal,Zola, Tolstoy, Gorki and Others*. London: Merlin Press

Mavisi, R. (2007). Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Kazi za Zainabu Burhani Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Mbogo, E. (2002). *Watoto wa Mama Ntilie*. Dar es Salaam. HEKO Publishers Limited

Mboneko, K. (2004). *Pambazuko Gizani*. Dar es Salaam. E&D Limited

Mburu, S. (2016). When your man is a stay-at-home dad. *Daily Nation.* *https://www.nation.co.ke* (Accessed on 10th November 2018)

Mishra, G. (2004). Globalisation and Culture. Online Journal of Radical Ideas. *http//iis-db-Stanford.edu* (Accessed on 18th November 2016)

Mohamed, S. (1999). Defamiliarisation and Experimentation in The Kiswahili Novel: A Case Study of Kezilahabi's Novel: *Nagona* (Hotuba isiyochapihswa ya Uprofesa chuo kikuu cha Bayreuth)

Mohamed, S. na King'ei, K. (2008). *Posa za Bikisiwa*. Nairobi. Sasa Sema

Morrell, R. (2005). Foreword to Men Behaving Differently.In: Reid, Graeme and Liz Walker(eds) *South African Men Since 1994*.CapeTown: Double Storey

Morris, P. (2003). *Realism*. London. Routledge and Keegan Paul Ltd

Mrina B.F. na Mattoke,W.T. (1980). *Mapambano ya Ukombozi wa Zanzibar*.Dar es Salaam:Tanzania Publishing House

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Vitabu vya Said A. Mohamed**."** Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Mutembei, A. (2013). Hali na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili katika Tanzania. Makala katika *presstz.net* (Accessed on 15th April 2017)

Mwirabua, A. (2014). Ukoloni Mamboleo na Utandawazi Katika Tamthilia Teule.Tasnifu Ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Ndungo, C. (1985). Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi

Nnamdi, U. (2016). *Navigating Nkrumah's Theory of Neo-Colonialism in The 21st Century* E-International Relations Students

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*.Rock Island Augustana College

O'Connor, R. (2015). Depressed Parents and the Effects on Their Children. Psych Central. http://psychcentral.com (Downloaded on 20th April 2017)

Oni, A. (2003). Globalisation, Its Implications and Consequences for Africa. *International Journal of Africa&American Studies Vol 4. No. 2*

Otite, O. (1994). *Sociology: Theory and Applied*. Lagos: Malthouse Press Limited

P'Bitek, O. (1966 & 1967). *Song of Lawino and Song of Ocol*. London: Heinemann

Raheem, S. na Asim, M. (2015). Cultural Globalisation and Its Impacts on Students in Socio-Economically Backward District of Pakistan During 21st Century. *Journal of Siberian Federal University* pg 2152-2161

Salisu, S. (2004). Globalization as Neo- Colonialism.Human Rights, Neocolonialism and Imperialism in Nigeria. *Panorama*. https://www.tigweb.org (Accessed on 15th April 2017)

Scheidenhelm, C. (2007). American Literary History: Romanticism, Realism and Naturalism. Ph.D. Thesis. University of Loyola, Chicago

Senkoro F.E.M. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*.Dar es Salaam University Press

Shaka, J. (2013). Impact of Globalisation in Africa. *The Star*. https://www.the.star.co.ke (downloaded on10th November 2016)

Siraji, A. (2007). *Children in the Age of the Internet.* Riyadh. Al-Rushd Library

Sirucha, B.M. (1986). Hadhi na Hali ya Mwanamke Katika Riwaya za S.A.Mohamed**.** Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Snow, C. P. (1968). *The Realists*: *Portraits of Eight Novelists*. Macmillan ISBN

Stout, H. (2012). Stay-At-Home-Dads Are the New Status Symbol for Alpha Women. *Pacific Magazines Australia*. (Downloaded on 10th November 2016)

Symon, N. (1999). Men and Masculinity- The Presentation of Men and Relationships in Three Contemporary British Novels. M.A.Thesis.University of Berlin. Munich:GRIN Publishing

Tannen, D. (1990). *You Just Don't Understand:Women and Men in Conversation*.New York:Harper Collins Publishers

Tomlinson, J. (1999). *Globalization and Culture*. University of Chicago Press

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.Nairobi. Oxford University Press

United Bible Societies (1952) *The Holy Bible in Kiswahili Version*. Nairobi na Dodoma

Ulomi, O. (2006). *Pesa za Mawe*. Dar es Salaam. E&D Limited

Villanueva, D. (1997) *Theories of Literary Realism*. New York: State University of New York Press

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi***.** Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Walby, S. (1990). *Theorising Patriarchy*.London:Basil Black Well

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi:Misingi na Vipengele vyake*.Nairobi:Phoenix Publishers

Wamitila, K.W. (2007). *Mwongozo wa Mwisho wa Kosa*, Nairobi. Vide muwa

Wamitila, K.M. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi.Focus Publishers

Wandera, S. (2002). **"**Utafiti wa maswala ya Kijinsia Katika Kiswahili**."** Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret:Moi University Press

Wa Thiong'o, N. (1972). *Home Coming*. Heineman Educational Books

Winerman, L. (2005). Helping Men to Help Themselves. *http://www.apa.org* (Accessed on 12th August 2017)

World Economic Forum (2016). *Global Competitiveness Report* 2015-2016 *http://reports.weforum.org*